Basi enendeni mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi.
Mathayo 28:19

# Njia ya Uanafunzi

# Orodha ya Yaliyomo


| Somo | | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1. | Njia ya Uanafunzi | 3 |
| 2. | Uchaguzi wa Wanafunzi | 6 |
| 3. | Kufanyiza kwa Wanafunzi kwa Uwepo wa Yesu | 9 |
| 4. | Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mafundisho ya Yesu (Sehemu ya 1) | 12 |
| 5. | Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mafundisho ya Yesu (Sehemu ya 2) | 15 |
| 6. | Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mafundisho ya Yesu (Sehemu ya 3) | 18 |
| 7. | Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mahusiano ya Kibinadamu | 21 |
| 8. | Mazoezi ya Uanafunzi Kulingana na Uhusiano na Ulimwengu | 24 |
| 9. | Uzazi na Kufanyiza/Malezi ya Wanafunzi | 27 |
| 10. | Uzazi wa Wanafunzi | 30 |
| 11. | Kanisa Ni Nini? | 33 |
| 12. | Sifa za Kanisa | 36 |
| 13. | Kichwa cha Mwili | 39 |
| 14. | Karama za Kiroho | 42 |
| 15. | Kazi ya Kila Kiungo | 45 |
| 16. | Kuwakamilisha Watakatifu | 49 |
| 17. | Kukihudumia Kichwa | 52 |
| 18. | Huduma kwa Mwili | 55 |
| 19. | Huduma Yetu kwa Ulimwengu | 58 |
| 20. | Ukomavu Katika Kristo | 61 |

# Somo la 1

## Njia Ya Uanafunzi

Lengo la somo hili: Ili kuonyesha kuwa uanafunzi si kufikia lengo na kubakia hapo, bali badala yake ni njia ambayo inasonga mbele katika malengo mapya katika kuendelea kwetu kujifunza.

### Njia ya Uanafunzi

1. Biblia inatuonyesha jinsi ambavyo uanafunzi unaanza. Soma Mathayo 4:19-20. Yesu akawaona Petro na Andrea wakivua akawaita. "__________________, nami nitawafanya kuwa ___________________. Mara wakaziacha nyavu zao, _________________________ ."
2. Yesu aliwaita wamfuate Yeye naye Petro na Andrea wakafanya hivyo. Ili kumfuata Yesu ilibidi waamue kumfuata Yeye. Kulingana na mstari wa 20, hili lilimaanisha kuziacha nyavu zao na kumfuata Yeye. Uamuzi huu wa awali katika uanufunzi una matokeo mazuri na mabaya. Kulingana na mstari wa 20, ni nini ilikuwa tokeo baya? __________________________ nyavu zao. Ni nini ilikuwa tokeo zuri? ________________________ Yesu.
3. Tokeo baya katika uamuzi wa awali katika uanafunzi ili kuwa kuziacha nyavu zao, na upande mzuri ilikuwa ni kumfuata Yesu. Kila mtu ili awe mwanafunzi wa Yesu, lazima aache kitu fulani ili amfuate Yeye. Kama tayari wewe ni mwanafunzi wa Yesu, umeacha nini ili umfuate Yeye? ____________________________________________________________
   Kama wewe si mwanafunzi wa Yesu, ingekupasa kuacha nini ili umfuate Yeye? ____________________________________________________

### Kufanyika kwa Mwanafunzi

4. Mwanafunzi/mfuasi ni mwanafunzi, na mwanafunzi anahitaji mwalimu. Katika suala hili, mwalimu ni Yesu. Katika Injili ya Marko tunaambiwa kuwa Yesu aliwaweka wakfu kumi na wawili ili wawe pamoja na Yeye. Uanafunzi ni mahusiano ya karibu sana na Yesu. Soma Mathayo 11:28-30. Yesu alisema, "Mjifunze __________________." Yesu anatamani kwamba mwanafunzi ajifunze kuwa kama Bwana wake. Kama Bwana ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, mwanafunze anatakiwa kuwa ________________ na _______________ wa moyo pia.
5. Ndiyo, mwanafunzi anahitaji kujifunza kutoka kwa Mwalimu mpaka anakuwa mpole na mnyenyekevu kama Mwalimu. Katika tukio lingine,

Yesu alilinena hili kwa wazi sana. Soma Mathayo 10:24-25. Yatosha kwa mwanafunzi kuwa kama Bwana wake, na mtumishi kuwa kama bwana wake. Wanafunzi walikuwa pamoja na Yesu kwa miaka, wakiyasikia anayoyasema, wakiyatazama anayoyafanya, na kwenda pamoja naye popote alipokwenda.

6. Wanafunzi si tu walikuwa na uhusiano na Yesu, lakini pia na wanafunzi wengine. Wakati mwingine Yesu alizungumza na mwanafunzi mmoja, lakini kwa sehemu kubwa utendaji ulikuwa kwa kikundi. Kujifunza kutoka kwa Yesu maana yake kujifunza kuishi katika jamii pamoja na wengine. Kujifunza kuishi kama kikundi haikuwa rahisi. Soma Mathayo 18:1-5. Kulikuwepo na ushindani na wivu kati ya wanafunzi. Kila mmoja alitaka kujua ni nani atakayekuwa ____________________________ katika ____________________________ wa mbinguni. Hata kati ya wanafunzi, Ilimpasa Yesu ashughulike na suala la shauku binafsi.
7. Ili kulijibu swali la ni nani atakayekuwa mkuu kuliko wote katika ufalme, Yesu alifundisha kuwa mkuu ni yule mwenye kujidhili nafsi na kuwa kama __________________. Unyenyekevu wa kweli ni ufunguo wa mahusiano mema ya kibinadamu. Mahusiano binafsi mabaya karibia wakati wote chanzo chake ni kiburi. Unyenyekevu unatafuta kundi kuwa vyema badala ya kuweka mkazo juu ya mtu mmoja. Hata Yesu ameliweka hili wazi kuwa unyenyekevu ni hitaji la kuingia katika Ufalme wa Mungu. Hotuba ya Mlimani, iliyotolewa na Yesu, inaiweka wazi tabia ya mwanafunzi. Ni kuwa mwanafunzi ni raia wa Ufalme wa Mungu, na kwa sababu hiyo, anajinyenyekeza yeye mwenyewe mbele za Mungu. Ni nini sababu ya matatizo kati ya Wakristo? __________________________________________
.
8. Wakati Yesu alipowaita wanafunzi wake. Aliwaambia kusudi la uanafunzi. Walikuwa wavuvi, akawaambia kuwa atawafanya kuwa _______________________ wa watu. Yesu aliwafundisha wawe wavuvi wa watu kwa kuwafundisha ukweli, kwa kuidhihirisha nguvu yake, na kwa kuwatuma kwenda kuhubiri. Uanafunzi haukuwa mpango wa masomo ya dhana isiyo na kusudio, lakini ni harakati yenye matendo. Yesu hakuwafungia wanafunzi ndani ya darasa kila siku, lakini aliwapeleka pembezoni mwa njia, milimani, katika maziwa, mijini, na katika majiji. Ni ipi ingekuwa ndiyo njia bora ya kuwa mvuvi wa watu-kubakia darasani au kutoka na kuwa kati ya watu?

_________________________________________________________________
.
9. Kabla ya kuondoka katika ulimwengu huu, Yesu alitoa maelekezo yake ya mwisho na yaliyo muhimu kwa wanafunzi wake. Soma Mathayo 28:19, 20. Basi enendeni mkafanye mataifa yote _________________________________. Kuwa mwanafunzi ina maana kufanya wengine kuwa wanafunzi. Wanafunzi hawakutakiwa kupokea

wasaa na ahadi za Ufalme wa Mungu ili tu wazifurahie wenyewe, bali waifikishe injili ulimwenguni pote. Kufanya wanafunzi kunahitaji utoke ubatize na kufundisha yote ambayo Yesu ameyafundisha. Ubatizo wa maji ni ushuhuda wa uamuzi thabiti wa kujifunza na kumfuata Yesu. Mwanafunzi aliyekomaa ana wajibu wa kufundisha wanafunzi wapya mafundisho yote ya Yesu. Nini hutokea ikiwa mtu anasema yeye ni mwanafunzi, lakini hafanyi wanafunzi wapya?

______________________________________________________________
.

**Lengo la Uanafunzi**

10. Kabla tu hajaondoka, Yesu alisema, Tazama nipo pamoja nanyi hata ________________________. Yesu amemtuma Roho Mtakatifu ili kuwapa wanafunzi uwezo kila siku. Mwanafunzi yupo njiani katika kufanywa kuwa kama Yesu, hadi kufikia kimo cha utimilifu wa Kristo. (Waefeso 4:13) Mwanafunzi mwaminifu hataridhika kubakia papo hapo tu. Baadhi ya Wakristo hawasogei baada ya kuwa wamefanya uamuzi wa "kumkubali Kristo." Wengine wanakuwa washirika tu, lakini washirika wa kanisa wasio na utashi wa kutenda. Washirika wengi wa kanisa hata hawamruhusu Roho Mtakatifu awatumie kufanya wanafunzi wapya. Mwanafunzi wakati wote atashughulika katika kulifikia lengo hili. Soma 1 Yohana 3:2: (Kristo) atakapotokea, tuta ____________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Baadhi wanauangalia uanafunzi katika hali ya kiinjilisti tu na kufikiria kuwa kuwafanywa kwao si muhimu sana. Kwa namna hiyo wana wengi waliofanya maamuzi kwa ajili ya Kristo, lakini wanafunzi wachache. Ni nini kifanyike katika hali hii?

2. Wengine wanauangalia uanafunzi kama namna ya taratibu za muundo, na wanasahau hali ya kujizalisha. Hili linaweza kutatuliwaje?

3. Washirika wengi wa kanisa ni mashibiki tu wasio na utashi wa kutenda badala ya kuwa washiriki watendaji katika kazi. Ufumbuzi wa tatizo hili ni nini?

## Somo la 2

## Uchaguzi wa Wanafunzi

Lengo la Somo: Kuzielewa tabia za watu ambao Yesu aliwachagua wawe wafuasi wake.

1. Ili kujua jinsi ambavyo Yesu alichagua wanafunzi wake, unaweza kusoma katika Mathayo 4:17-20. Yesu aliwahubiria toba makutano kama hatua ya kwanza ya kuuweka utawala wa Mungu katika maisha ya wasikilizaji wake. Ni wazi kuwa Yesu alianza huduma yake kwa kuhubiri toba kwa makutano. (Luka 4:14-15) Yesu alihubiria nini makutano? ____________ ____________________________________________________________
2. Yesu aliwahubiri toba makutano. Pia alitangaza kuwa ufalme wa Mungu umekaribia. Mtazamo wa ufalme wa Mungu ina maana kuwa Mungu anaanza kutawala katika maisha ya wale wenye kutubu. Mtu mwenye kutubu anatambua kuwa Yesu ndiye mtawala wa maisha yake; huo ndio mwanzo wa maisha ya uaminifu kwa Yesu. Toba maana yake Yesu amekuwa ______________ wa maisha yako. Je! umemruhusu Yesu kuwa mtawala wa maisha yako? ________________________________________
3. Kulingana na mstari wa 18, Yesu aliwaona Petro na Andreda wakizitupa nyavu zao baharini kwa sababu walikuwa ni _________________________. Yesu akawaita hawa wavuvi wawe wanafunzi wake. Ni muhimu kuona kuwa Yesu aliwaita watu waliokuwa watenda kazi wenye kuwajibika. Yesu hakutafuta watu wenye nafasi za juu katika jamii, lakini hata hivyo hakutafuta watu wasiowajibika. Yesu alichagua aina gani za watu? ___________________________. Unafikiri ni kwa nini Yesu alichagua aina hizi za watu ili wawe wanafunzi? __________________________________.
4. Ni dhahiri kuwa Yesu alichagua watenda kazi kwa sababu alitamani watu wenye kuweza kufanya maamuzi na kujitoa ambao wataweza kutekeleza matakwa ya uanafunzi. Katika nyakati zingine, kuna jaribu la kutafuta watu wasiofanya lolote tukifikiri kuwa watakubali kupewa injili kwa urahisi. Kama tukiwapa kitu fulani chenye kuvutia, labda watakikubali. Lakini, ni nini kitakachotokea kama tukiwapa watu injli ambao hawana shughuli/ajira na wenye mahitaji? Jibu kulingana na mawazo yako mwenyewe kuhusu hili. ____________________________________________________________.
5. Mara nyingi hutokea kuwa wasio na shughuli/ajira na wenye mahitaji wanaoikubali injili wanakuwa wenye kuwategemea wengine. Badala ya kuiwakilisha injili kama kitu cha kuchagua kwa hiari Yesu aliiwakilisha kama kitu kinachohitajika. Katika mstari wa 19, Yeye alisema, Mnifuate. Hii ni aina ya sharti. Ni amri. Yesu, Bwana ananena kwa amri na sisi.

Kulingana na mstari wa 20, Petro na Andrea walifanya nini?

______________________________________.

6. Waliziacha nyavu zao wakamfuata yeye. Lazima tusifikiri kuwa walilazimika kufanya kitu kinyume na utashi wao. Injili kulingana na Yohana inaelezea kuwa Andrea alimsikia Yohana Mbatizaji akimwakilisha Yesu kama Mwana Kondoo wa Mungu. Kwa hiyo Andrea akaanza kumfuata Yesu. Baadaye alimleta Petro kwa Yesu. Kwa hiyo ni wazi kuwa Yesu aliwakilisha matakwa ya uanafunzi kwa watu waliokuwa wameonyesha uamuzi wa kumfuata Yeye. Je! unadhani Petro na Andrea walilazimishwa kumfuata Yesu? ______________________________. Kwa nini walimfuata Yesu mara moja?

   ____________________________________________________________.

7. Petro na Andrea hawakulazimika kumfuata Yesu, lakini waliyaitikia matakwa ya uanafunzi kwa hiari. Ni wazi kuwa si wote walioitwa wameteuliwa. (Mathayo 22:14) Soma Mathayo 8:19-22. Mwandishi katika kifungu hiki amejieleza kwa ufasaha sana. Anaonekana kuwa anajithatiti pasipo kuwa na masharti. Lakini Yesu aliitikia kwa kuyaweka wazi dhiki na magumu ya kuwa mwanafunzi kwa kusema kwamba Mwana wa Adamu hana mahali pa ____________________. Yesu alimjibu vipi yule mtu aliyetaka kufanya kitu fulani kwanza ndipo amfuate Yeye?

   _____________________________________________________________

8. Wakati Yesu alipochagua wanafunzi wake, Ilibidi awaondoshe baadhi. Lakini Yesu hakuwaondosha moja kwa moja wale waliojitoa wenyewe kwake kijuu kijuu kwa ajili ya uanafunzi. Yeye alionyesha tu matakwa na magumu ya kuwa mwanafunzi, na wale watu ambao hawakuwa na utayari wa kuikubali changamoto walijiondoa. Hili ndilo lilifanya tofauti kati ya makutano ya wasikilizaji na kundi dogo la wanafunzi. Roho ya makutano ilikuwa na tofauti. Yesu aliwalisha wale elfu tano kimuujiza. Siku iliyofuata watu wengi walimtafuta Yesu. Lakini Yesu aliutambua mtazamo wa watu. Soma Yohana 6:26-27. Kwa nini watu walimtafuta Yesu? _________________. Yesu aliwaambia watu watafute aina gani ya chakula?

9. Yesu aliwataka watu wasitafute tu chakula cha duniani au cha asili) bali chakula cha milele. Alipowaambia kuwa lazima waule mwili wake, wengi hawakuweza kuelewa, wakajiondoa. Halafu Yesu akaongea kwa karibu sana na wanafunzi wake. Soma Yohana 6:67. Yesu aliwauliza wanafunzi wake wa karibu kuliko wote kama nao walitaka kuondoka pia. Ni muhimu kuona kuwa Yesu hakuwasihi wabaki, lakini Yeye alilisubiri tu jibu la ujasiri na la mara moja kutoka kwao. Walimjibuje? _______________

   ____________________________________________________________.

   Unafikiri lipi ni bora zaidi: kuwasihi watu kukubali yale Mungu anayowapa, au kuwatia changamoto na matakwa ya uanafunzi? Elezea maoni yako. ______________________________________________

   ____________________________________________________________.

10. Kwa njia fulani, Injili inatoa kitu chenye kuvutia, lakini ili kufanya wanafunzi walio imara ni lazima kuyakabili matakwa ya uanafunzi. Lazima tukumbuke kuwa Yesu hakuacha kufanya kazi na makutano, lakini alijua kwa hakika kuendelea kwa kazi kunategemeana na kundi la watu waliochaguliwa ambao wangeweza kupewa nidhamu kwa kuambatana na Yesu katika uwanja wa utendaji. Kwa nini kundi la wanafunzi liundwe?

## Utendaji wa Kikundi

1. Wote wenye kuanza kujifunza uanafunzi wanatakiwa kujihesabu wenyewe kuwa ni wanafunzi ambao waliianza safari ya uanafunzi. Kila mtu katika kundi anatakiwa kulijibu hili swali: Kuwa mwanafunzi kuna maana gani kwangu?

2. Waamini wengi na washirika wa kanisa leo wanashindwa wapi katika uanafunzi wa kweli?

3. Tunaweza tukahusianisha vipi yale matoleo ambayo injli inatoa na matakwa ya uanafunzi?

## Somo la 3

## Kufanyiza kwa Wanafunzi kwa Uwepo wa Yesu

Lengo: Ipate mifano ya jinsi ambavyo Yesu alionyesha kwa matendo yale aliyoyafundisha kwa maneno.

1. Katika somo la kwanza, ulijifunza kuwa mwanafunzi anajifunza kutoka kwa Yesu sifa za upole na unyenyekevu. Njia bora ya kujifunza sifa hizi za tabia ni kwa kuyatazama matendo ya mtu mwenye kuzionyesha sifa hizi. Soma Mathayo 11:25. Yesu ametambua sifa hizi ni za lazima katika kupokea ufunuo wa kimungu. Ni nani ambaye hawezi kupokea ufunuo wa kimungu. Ni nani anayeweza kuupokea? ___________________________.
2. Kweli za kimungu zimefichwa kwa wenye hekima na zinaeleweka na kufunuliwa kwa watoto wachanga. Mtazamo wa Yesu ni kinyume na mtazamo wa kidini wa dunia. Watu wengi wa wakati ule na pia wa siku zetu wanaamini kuwa ufunuo wa kimungu unategemeana na maandalizi ya kielimu. Lakini Yesu anatuonyesha sisi kuwa mtazamo wa moyo ni wa muhimu zaidi kuliko maarifa makubwa. Soma Luka 2:46-47. Wakati Yesu alipokuwa mtoto wa miaka kumi na miwili, Akawa Hekaluni katikati ya ______________. Nao wote waliomsikia ______________ _____________ na ________________________________.
3. Yesu hata katika ujana wake, alipata kupendezewa na madaktari wa sheria kwa sababu ya akili ya kupita kawaida. Baadaye, madaktari wa sheria wakajihusisha katika mapambano na Yesu pale walipogundua kuwa akili ya Mwalimu huyu mnyenyekevu ni kubwa kuliko ya kwao. Yesu hakuwekea unanafunzi wake juu ya sheria au taratibu za ibada, lakini juu ya sifa za tabia. Soma Yohana 14:6. Yesu Mwenyewe aliweza kusema, Mimi ndimi ______________________, ______________________, na ______________________. Sheria zote za haki zilifanyika mwili katika maisha ya Yesu mwenyewe. (Mathayo 5:17).
4. Uanafunzi ni jambo rahisi sana, lakini ni kitu fulani cha ndani sana. Soma Yohana 1:38-39. Mwaliko wa Yesu katika mstari wa 9 ni rahisi sana. Yeye alisema tu: ___________________ na _______________________. Wakiwa wanamfuata Yesu na kuiangalia tabia yake, mwanafunzi akaanza kujifunza sheria za ndani sana za haki. Mwanafunzi aliweza kuona mahubiri yakitendewa kazi kabla ya kusikia kuhubiriwa kwa mahubiri. Ni lipi lenye matokeo zaidi, maisha mhubiri au mahubiri yake? ___________________ ______________________________________________________________.
5. Hata wazazi wanaweza kutambua kuwa watoto wao wanafuata namna ambavyo wazazi wao wanaishi zaidi ya yale ambayo wazazi wao wanafundisha kwa maneno. Kwa mfano, kama watoto wanagombana, na wazazi wanawakaripia na kuwaambia wasigombane, halafu lisaa moja

baadaye wazazi wanagombana, ni nini ambacho watoto watakikumbuka zaidi-je! kile ambacho wazazi wamesema, au walichokifanya? __________. Kwa nini? ______________________________________________.

6. Unajua jibu la swali lililopita. Ni pale tu kile tunachokisema na tunachokifanya vinapokuwa vinakubaliana ndipo panakuwepo na mafundisho yenye matokeo. Kwa sababu hii, Yesu alipalilia mahusiano ya binafsi sana na wafuasi wake. Mahusiano haya ya karibu sana ndiyo uwezo ulioleta nguvu katika huduma ya wanafunzi. Soma Marko 3:13-15. Darasa la Yesu wakati huu lilikuwa juu ya mlima. (Mara nyingi Yesu aliwachukua wanafunzi kutoka katika makutano.) Panasema kuwa aliwaweka kumi na wawili ili wawe ________________ na ______________. Ni baada tu ya kuwa wao kuwa pamoja na Yeye ndipo walipotumwa kwenda kuhubiri, kuponya na kutoa mapepo. Mara nyingi waamini wanajaribu kwa haraka kufanya kazi ya Mungu pasipo kuwa wamekuwa pamoja na Yesu vya kutosha hata kuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Ni nini hutokea pale tunapojaribu kufanya kazi ya Mungu pasipo nguvu ya Mungu? ________________________________________.
7. Ilibidi wanafunze waipate katika Yesu nguvu ya kufanya kazi ya Mungu. Kama ambavyo imetajwa, mtazamo wa makutano ulitofautiana. Lakini ili kuwaandaa wanafunzi. Wakaanza kushiriki katika huduma ya Yesu. Baada ya muda wa kuwa pamoja, Yesu akawatuma mahali pengi katika timu ya wawili wawili. Soma Mathayo 10:5-8. Yesu aliwaamuru wafanye hasa kama ambavyo yeye alikuwa akifanya. Amri ya Yesu kwao ilikuwa ni nini? Na katika kuenenda kwenu, _____________, mkisema, ____________ wa mbinguni ______________. _____________ wagonjwa, __________ wafu, _____________ wenye ukoma, toeni _______________ .
8. Huduma ya wanafunzi haikuwa kuhubiri tu, lakini pia kukutana na mahitaji mengine. Muda ulivyoendelea kuelekea ______________________________. Yesu alitoa muda zaidi kwa wanafunzi. Kuimarika na kuendelea kwa kazi yake kulilitegemea kundi hili la wanafunzi. Walifikia kujua kuwa Yesu ni nani, na baadhi yao walikuwa wameuona utukufu wake. Wakati huo huo, aliwaonya juu ya mateso yake yanayokuja ili kwamba wawe na uwezo wa kuyakabili mateso yaliyokuwa yakiwangojea. Ni nani aliyeendelea na huduma ya Yesu baada ya Yeye kuondoka katika dunia hii? ____________________.
9. Wanafunzi ambao walikuwa wamekuwepo pamoja na Yesu waliiendeleza kazi ya Yesu. Kama Yesu angekuwa hajaliaandaa kundi hili la wanafunzi, kazi ya Kristo ingekuwa imefikia mwisho. Kwa njia ya wanafunzi kazi ya Yesu ilifikishwa katika maeneo mengi. Hata tunaweza kusema kwamba sisi leo tumepokea Injili kwa sababu walikuwa wanafunzi waaminifu waliotupatia sisi ujumbe. Imewezekanaje kuwa kazi ya Bwana inaendelea leo? _________________________________________________________.

10. Leo kuna hitaji kubwa kwa wanafunzi ambao wamejifunza kuhusu Yesu waendelee na kazi ya Mungu. Sasa hatuna uwepo wa Yesu kimwili lakini Roho Mtakatifu yupo hapa ili atuandae kwa ajili ya kazi. (Mathayo 28:20) Soma Yohana 16:7, 13-14. Ni wazi kuwa uanafunzi wa leo unatekelezwa na kundi la watu wenye kuongozwa na Roho Mtakatifu. Matokeo ni yapi wakati Mtu fulani anapojaribu kufanya kazi ya Mungu pasipo msaada wa Roho Mtakatifu? ________________________________________
.

## Utendaji wa Kikundi

1. Ufunuo wa kimungu unategemea zaidi mtazamo wa unyenyekevu kuliko unavyotegemea maandalizi mengi. Ni ipi ndiyo ingekuwa njia bora ya kuandaa wanafunzi kwa ajili ya Yesu?

2. Hata ingawa hatuna uwepo wa Yesu kimwili, je! wanafunzi wa leo wanawezaje kujifunza kuhusu Yesu?

3. Kwa nini watu wengi wanaomkubali Yesu wanafeli kuendelea kumfuata Bwana Yesu kwa uaminifu? Tufanye nini ili kuitengeneza vizuri hali hii?

4. Je! Inawezekana vipi leo kufanya wanafunzi wa karibu ambao wataendelea?

# Somo la 4

## Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mafundisho ya Yesu (Sehemu ya 1)

Lengo: Zielewe sifa za tabia za Yesu ambazo zinaweza kuwa sifa za tabia za mwanafunzi.

1. Yesu aliyaishi yale aliyoyafundisha, na pia aliyafundisha yale aliyoyaishi. Leo katika siasa, ahadi hutolewa ili kushawishi watu, halafu ahadi hizo hazitimizwi. Pia, kuna maneno mengi ya kidini yanayozungumzwa yenye kunena mawazo makubwa ya haki, lakini kuna utekelezaji mdogo sana wa mawazo haya. Panaweza pakawepo na jaribu la kufikiri kuwa Yesu alikuwa mtu mwingine tu wa kidini. Lakini Yesu alikuwa tofauti. Maisha yake yalikuwa tofauti na mafundisho yake yalibadilisha watu. Soma Mathayo 5:1-3. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Heri walio __________________wa roho. Yesu aliuonyesha mtazamo wake pale aliposema Yeye ni mnyenyekevu wa moyo. Je! Unafikiri watu wengi wanaamini kuwa maskini wa roho ni nini? __________________________.
2. Ni wazi kuwa watu wanafikiri ni vizuri kuwa tajiri katika roho. Soma Mathayo 5:13-16. Wanafunzi wa Kristo walikuwa ni ____________________ ya dunia na…_______________________ ya dunia. Unyenyekevu huu unatakiwa kuonyeshwa kwa kuwatumikia wengine. Mara nyingi hata washirika wa kanisa hawaelewi unyenyekevu. Wanafikiri kuwa mtu mnyenyekevu anatakiwa kusema kuwa hawezi kufanya mambo mengi. Lakini mwanafunzi mnyenyekevu kweli kweli yeye ni chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu. Lipi linaonyesha unyenyekevu wa kweli, "Mimi sina uwezo sana; ingekuwa bora mtu mwingine afanye," au Mungu atanisaidia kufanya mambo makubwa"? ______________________________.
3. Mtu mnyenyekevu ndio mtu ambaye Mungu anaweza kumtumia sana. Mtu mnyenyekevu anakubali kujinyenyekeza kwa Yesu kama mtawala wake. Soma Mathayo 5:17-20. Yesu ameuonyesha unyenyekevu wake kwa kujinyenyekeza katika mamlaka ya Baba yake. Hii ilikuwa namna yake ya kuonyesha kuwa hakuja kuiharibu torati bali __________________________. Mwanafunzi wa Yesu pia naye hujinyenyekeza katika mamlaka hii. Yeyote mwenye kuvunja moja ha hizi amri ataitwa __________________________ katika ufalme. Hili linathibitisha kuwa tumekuwa tukijifunza mtu mnyenyekevu ni mkuu katika ufalme wa Mungu.
4. Soma heri ya pili katika Mathayo 5:4. Hili pia ni fundisho lenye kuleta mapinduzi. Yesu alisema, Heri wenye _________________. Watu wanafikiri wale wenye kucheka ndio walio heri au wenye furaha. Wale wenye kulia (au kuomboleza) wanatambua makosa yao na kuyatubia. Yesu amesema wata_______________________. Lakini kuna usemi kuwa, "Wanaume huwa

hawalii. “Mawazo yako ni yapi? Je! Wanaume wanatakiwa kulia? ____________________. Wakati gani? ______________________________.

5. Wale wenye kulia na kuomboleza watapokea faraja na tulizo. Yesu mwanaume aliye mkuu kuliko wote, alilia wakati rafiki yake Lazaro alipokufa. Petro alitoa machozi baada ya kumkana Bwana wake. Biblia inatuambia kuwa watu wakuu walilia. Tunatakiwa kuomboleza juu ya makosa yetu ili tuishi maisha yaliyo bora. Yesu ametaja baadhi ya makosa yetu tuliyoyazoea. Soma Mathayo 5:21-26. Hasira ni chanzo cha matendo mengi ya fujo. Wakati tunapomletea Mungu sadaka, na kutambua kuwa tumemkwaza ndugu, tunatakiwa kufanya nini kwanza? ________________ ______________________________________________________________.
6. Yeye mwenye kuhuzunikia dhambi zake anayatambua makosa yake na kupatana na ndugu ambaye amemkosea, ndipo anaweza kuileta sadaka yake mbele za Mungu. Mwanafunzi wa kweli wa Yesu anataka kuwa na Amani na wanafunzi wengine. Lakini kuna makosa mengine. Soma Mathayo 5:27-32. Tamaa ni chanzo cha uzinzi. Aina hii ya kutokuwa mwaminifu ni nzito sana, na Yesu alisema kuwa ni afadhali kuteseka katika mwili kuliko kutokuwa waaminifu katika viapo vyetu vya ndoa. Bila shaka, kutendea vibaya miili yetu hakutatatua tatizo la moyo wenye tamaa. Moyo wenye kulia kwa kutubu kwa dhati unaweza kuokolewa kutoka katika kifungo hiki na kwa sababu hiyo utapokea tulizo. Ufumbuzi kwa tatizo la uzinzi ni nini? ________________________________________ ______________________________________________________________.
7. Mtu anatakiwa kutoa machozi ya toba kama alivyofanya Daudi, na kumruhusu Mungu ampe moyo mpya. Yeye mwenye kuomboleza kwa toba ya dhati anasafishwa katika moyo wake. Yesu ametaja dhambi nyingine mbaya sana itokayo katika moyo wenye dhambi. Soma Mathayo 5:33-37. Watu huzoea kudanganya kwa kusema uongo; huwa inakuwa hivyo kiasi kwamba mahakama za sheria huwa zinawataka wafanye kiapo. Lakini mtu ambaye ni mwongo yeye hatasema ukweli hata chini ya kiapo (Hilo linaitwa “perjury” au kosa la kusema uongo). Lakini Yesu si tu anakataza kosa la kusema uongo lakini anakataza pia ________________. Mtu ambaye husema kweli wakati wote hana haja ya kuapa kiapo. Kwa nini tusiape? ___________________. Kwa nini ni makosa kuvunja kiapo kwa kuambiana uongo? _____________________________________.
8. Soma Mathayo 5:5, heri ya tatu. Heri __________________ maana wata___________________ nchi. Watu wa ulimwengu wanafikiri kinyume na hili. Wanaamini kuwa njia ya kupata himaya zaidi ni kwa kupambana. Vita nyingi ni matokeo ya kutaka himaya zaidi na marupurupu ya kiuchumi. Mtu mpole anatafuta wengine wawe vyema. Soma Mathayo 5:38-39. Mtu mwenye kutazamia kisasi anatafuta kulipiza jicho kwa ______________ na jino kwa _______. Mwenye kisasi anataka hata meno kadha wa kadha ya adui yake kwa kila moja alilolipoteza.

Lakini mwanafunzi mpole, baada ya mtu kumpiga shavu moja, atageuza ________________________.

9. Soma Mathayo 5:40-42. Watu wa ulimwenguni wanafanya yale tu ambayo sheria inawataka wafanye, lakini mwanafunzi mpole yeye hatabeba tu mzigo maili moja lakini maili ____________. Hili lina maana kuwa mfuasi wa Kristo hatumikii kwa kulazimishwa, bali kwa hiari.
10. Soma Mathayo 5:43-48. Ni kawaida sana kwetu sisi kuwapenda wale wanaotupenda, lakini mwanafunzi mpole wa Yesu anatakiwa kuwapenda ________________ wake pia. Haiwezekani kuzitii amri za Bwana pasipo upendo wa Bwana katika mioyo yetu. Ni dhahiri kuwa Yesu anatarajia mwanafunzi adai kwa ajili yake mwenyewe sifa zile zile alizozionyesha Yesu. Mwanafunzi afanye nini wakati kuna migogoro kati ya majirani? _______ _________________________________. Na migogoro kati ya mataifa? ___________________________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Sisi tuko tofauti na ulimwengu, lakini tunatakiwa tuwalete kwa Kristo. Je! twawezaje kuwa tumejitenga na uovu na bado tukawapata wenye dhambi?

2. Tunawezaje kuwa chumvi na nuru katika jamii yetu?

3. Lipi ni baya zaidi-hasira, uzinzi au udanganyifu? Inawezekana kuyaondoa maovu haya kwa jinsi gani?

4. Ni kwa njia gani kanisa linaweza kuionyesha jamii kwamba sisi tutabeba mzigo wao hata maili ya pili?

5. Tunawezaje kuuonyesha ushuhuda wetu kwa wenye mamlaka kuhusu utumishi wa umma ambao unatumia fujo dhidi ya binadamu?

# Somo la 5

## Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mafundisho ya Yesu (Sehemu ya 2)

Lengo: Zielewe sifa za tabia zilizo katika Yesu ambazo zinatakiwa kuwa sifa za tabia za mwanafunzi.

1. Soma heri ya nne katika Mathayo 5:6. Kama tunataka kushibishwa na kutoshelezwa, lazima tuwe na ______________ na _____________ ya haki. Tunajifunza kutoka katika maisha ya asili kuwa hata watoto wanataka kula pale wanapokuwa na njaa. Mwanafunzi ana njaa na kiu ya haki. Lakini Yesu anatoa onyo kuhusu kufanya matendo yetu ya haki ili tu kuwashawishi wengine. Soma Mathayo 6:1-4. Wanafiki huwa wanafanya nini wakati wanapotoa sadaka kwa maskini? _________________________. Kwa nini wanafanya hivyo? _____________________________. Sadaka zetu zitolewe jinsi gani ili tuweze kupokea thawabu toka kwa Mungu? ____________________________________________________________.
2. Soma Mathayo 6:5-6. Kwa nini wanafiki wanapenda kusimama kusali mbele ya wengine? Ili ________________ mbele ya __________________. Maombi ni kukutana na Mungu kwa karibu sana, na tunatakiwa kukumbuka kuwa katika maombi tupo katika uwepo wa Mungu. Maombi ya ndani kabisa hufanywa wakati tuko peke yetu na Mungu. Kuomba kwetu kwingi zaidi tukufanye wapi, nyumbani au katika ibada za kanisa? ______________________________. Yeye mwenye kuomba akiwa na njaa na kiu ya haki ana shauku naye ataipokea thawabu yake toka kwa Mungu.
3. Soma Mathayo 6:7-13. Kama maombi ni utendaji wa kidini tu, yanaweza kuwa maneno tu na marudio batili. Je! unajua maombi matupu? __________________. Yakoje? ________________________. Lakini Mungu anajua mahitaji yetu hata kabla hatujamwomba. Maombi yanapashwa kuwa mazungumzo na Bwana ambapo hatuzungumzi naye tu, bali pia tunamsikiza. Itafakari Sala ya Bwana. Katika sala hii, mwanafunzi mwenye njaa anaomba kwamba ______________________________ uje, na kwamba ______________ ya Mungu yafanyike. Ni baada tu ya kujinyenyekesha katika mapenzi ya Mungu ndipo tunaweza kuomba mkate/ riziki yetu ya _______________. Katika maombi yetu, tunatakiwa kuelezea nini kwanza, sifa zetu kwa Mungu, au haja zetu? ______________ ____________________________________________________________.
4. Soma heri ya tano. Wenye rehema wanapokea __________________. Kama tunataka kupokea rehema, tunatakiwa tuwafikishie rehema wengine. Tunapoirudia Sala ya Bwana, tunasema kitu kile kile tunaposema, Utusamehe dhambi zetu, kama nasi tunavyo______________________ wale walio________________. Pia soma Mathayo 6:14-15. Kama

tunawasamehe wengine, _____________ wetu atatusamehe sisi pia _______________ zetu. Hili linatuonyesha kwamba Mungu anataka wanafunzi wake wawe na mahusiano mema wao kwa wao.

5. Wakati mwingine tunapokuwa na mgogoro binafsi ni ngumu kusamehe. Wakati watu wawili wanapojisikia wamekosewa, mmoja anamsubiri mwingine achukue hatua ya kwanza ya upatanisho. Lakini Mathayo 5:23-24 inasema aliyekosea achukue hatua ya kwanza ya upatanisho, na 18:15 inatwambia sisi kuwa aliyekosewa achukue pia hatua za kwaza za upatanisho. Katika namna yako ya kufikiri, ni nani anayetakiwa kutafuta upatanisho, aliyekosea au aliyekosewa? ___________________________.
6. Soma heri ya sita katika Mathayo 5:8. Ni nani atakayemwona Mungu? Wenye _______________. Wenye moyo safi ni wale wasiotiwa doa na kitu fulani kinyume na mapenzi ya Mungu. Soma Mathayo 6:16-18. Mwanafunzi anayefunga kwa dhati anaweka mkazo juu ya mapenzi ya Mungu pasipo kupotoshwa na shauku zake mwenyewe za kimwili, chakula au shauku binafsi. Mathayo 17:21 inatwambia sisi kuwa kufunga na maombi kunaweza kumsaidia mwanafunzi kuikamata nguvu ya Mungu ili kutoa mapepo. Je! unalijua tukio katika siku zetu ambapo kufunga ilikuwa baraka? ____________________________. Elezea kwa kifupi. ________ ________________________________________________________.
7. Soma Mathayo 6:19-23. Mwanafunzi mwenye moyo safi ataweka thamani sahihi juu ya mali. Ni nini hutokea katika hazina (mali) zetu za duniani? ____________________. Je! Katika hazina tunazoziweka mbinguni? ________________________. Moyo wa mwanadamu unathamini yale ambayo macho yanayatazama. Ni kweli hazina za duniani zinaweza kuwa na thamani, lakini ni thamani ya kitambo tu. Tunapofikia mwisho wa maisha, ni nini kitakachokuwa hazina yenye thamani ya kudumu? ____ ________________________________________________________.
8. Soma Mathayo 6:24-26. Mwanafunzi mwenye moyo safi hataugawa uaminifu wake kati ya mabwana wawili, kwa sababu Yesu ni Bwana na Mkuu wake. Ni nini hutokea wakati Mkristo anapojaribu kutumikia mabwana wawili? Mkristo anayejaribu kumtumikia Mungu na utajiri hamwamini Mungu amtunze. Yesu hashutumu kazi ya dhati, bali fadhaa na kuwa na wasi wasi tu. Je! Kazi ni mbaya? _______________. Je! fadhaa ni dhambi? _________________________________________.
9. Soma Mathayo 6:27-32. Mungu atoa mahitaji kwa ndege wa angani, maua ya kondeni na kwa ajili ya majani ambayo huwa hai kwa muda mfupi. Wasi wasi hauleti matokeo mazuri. Je! inawezekana kujiongezea chochote katika kimo chetu kwa wasiwasi na fadhaa? _______________. Kweli kweli hakuna sababu yeyote ya sisi kuwa na wasi wasi, kwa sababu Baba yetu wa mbinguni anajua tunayoyahitaji kabla hatujaomba (Mathayo 6:8, 9). Kama Baba yetu wa mbinguni anatunza mimea, je! si zaidi sana

atatutunza sisi? Kwa mwanafunzi mwenye moyo safi, Mungu si tu Yeye ni Bwana na Mkuu wetu, lakini Yeye pia ni ________________________ mwenye kututunza.

10. Soma Mathayo 6:33-34. Kuwa na utunzaji wa Baba yetu ni fursa ya wale walio kwenye Ufalme wa Mungu. Tunatakiwa tuutafute Ufalme wa Mungu wakati gani: kabla au baada ya mambo mengine yote? _________________. Baada ya kuutafuta Ufalme wa Mungu na haki yake, kuna ahadi gani? Tuta __________________________________________ mambo haya yote.
11. Mungu anaahidi kukutana na mahitaji ya mtu ambaye amejinyenyekeza katika utawala wa Mungu. Mara nyingi kuna watu wajiitao wenyewe kuwa ni Wakristo ambao wanajaribu kusaidia mipango ya faida za kiuchumi na maendeleo kwa ajili ya wale ambao hawajayanyenyekeza maisha yao katika ubwana wa Yesu. Mara nyingi, watu hawa huuchukua msaada walioupokea na huutumia kutegemeza tabia zao mbovu. Je! binafsi unawajua watu ambao wamefanikishwa baada ya kuwa wamejinyenyekeza katika ubwana na mapenzi ya Mungu? ____________________________. Toa ushuhuda mfupi wa mtu wa namna hiyo. ______________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Elezea jinsi ambavyo Mungu ametosheleza njaa na kiu katika maisha yako mwenyewe.

2. Je! unafikiri Mungu huwa anasikia marudio-rudio yetu yaliyo batili? Je! huwa anayajibu?

3. Je! Mwanafunzi wa Yesu anaweza kusema, “Mimi siwezi kumsamehe ndugu yule kwa sababu kosa lake lilikuwa kubwa sana?” Ni nini hututokea kama hatumsamehi ndugu yetu?

4. Je! ni vibaya kuwa tajiri? Kwa nini ni hatari (hasa kwa Mkristo)?

## Somo la 6

## Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mafundisho ya Yesu (Sehemu ya 3)

Lengo: Kuendelea kuzielewa sifa za tabia ya Yesu ambazo zinatakakiwa ziwe sifa za tabia ya mwanafunzi.

1. Katika somo hili utajifunza kuhusu sifa katika maisha ya Yesu ambazo pia zinatakiwa ziwe sifa za tabia ya mwanafunzi, kama ambavyo imeelezewa katika heri zilizopita na katika sehemu ya mwisho ya Hotuba ya Mlimani. Soma Mathayo 5:9. Ni kina nani watakaoitwa wana wa Mungu. ______________. Leo kuna migogoro kati ya mataifa, majirani na wakati mwingine hata kati ya ndugu. Mwanafunzi anayejua jinsi ya kuwa mpatanishi ataweza kuwa na huduma kubwa. Kuna vitabu vingi na kozi kuhusu mahusiano ya binadamu. Unafikiri ni kina nani wanaotakiwa kuwa Wapatanishi walio bora? ____________________________________.
2. Soma Mathayo 7:1-2. Kama sisi tu wepesi kuhukumu wengine, nasi pia tuta______________________. Ni kibinadamu sana kuhukumu wengine kwa hukumu kali wakati huo huo tunakuwa na upole juu ya nafsi zetu. Lakini kulingana na mafundisho ya Yesu, wote tutapimwa kwa __________________ ile ile. Kiujumla duniani kuna kiwango kimoja cha haki kwa ajili ya watu wa cheo cha juu kijamii au kiuchumi, na kingine kwa ajili ya watu ambao ni maskini na wenye nafasi chache za kuishi vyema. Je! Mpatanishi halisi anaweza kutambua viwango tofauti vya haki kwa njia hii? _______________. Kwa nini? _________________________.
3. Soma Mathayo 7:3-5. Ingekuwa la kufurahisha kiasi gani kumuona mtu mwenye boriti kubwa jichoni pake akijaribu kufanya kazi makini ya kuondoa ______________ kutoka katika jicho la mtu mwingine! Je! ni makosa kujaribu kutoa doa kutoka katika jicho la ndugu yako? _____________. Lakini tufanye nini kwanza? ______________________. Mara nyingi matatizo ambayo ni dhahiri zaidi na ambayo tunayahukumu zaidi katika maisha ya wengine, ndiyo matatizo yayo hayo tulionayo wenyewe. Mpatanishi huyanyoosha maisha yake mwenyewe kwanza kabla ya kusahihisha wengine.
4. Soma Mathayo 7:6. Je! unafikiri ghuruwe wangekuwa makini na lulu za thamani? _______________. Kwa nini? _________________. Ingawa tunatakiwa kuwa makini kutokuwaelewa wengine vibaya, mstari wa 5 unafundisha kwa wazi kuwa tupambanue. Kuna mambo ambayo ni matakatifu sana na ya thamani hata hatutakiwi kuwatupia wale ambao watayaharibu-haribu na kuyakanyaga. Katika siku zile palikuwepo na watu wa kidini ambao waliikufuru kazi ya Roho Mtakatifu kwa kusema kwamba Yesu alitoa mapepo kwa nguvu ya ibilisi (Beelzebuli). Tunatakiwa

kumshirikisha nani uzoefu wetu wa ndani sana na wa thamani na Bwana? ______________________________.

5. Soma Mathayo 5:10. Watu wa ulimwenguni wangesema, "Heri wenye kupendwa na wengi, "Lakini Yesu anatangaza: Heri wenye __________ kwa ajili ya ________________. Kuna wengi wenye kuteseka kutokana na udhalimu wao wenyewe, lakini ni wachache kiasi wenye kuteseka kwa ajili ya haki. Paulo ameandika kuwa wale watakaoishi kwa utauwa katika ulimwengu huu watapata mateso (2 Timotheo 3:12). Kwa Wakristo wengi leo, maisha ya Kikristo ni ya raha sana, na sababu hiyo kwa kawaida huwa wanajaribu kuepuka aina yeyote ya mateso. Kwa nini kuna mateso kidogo siku hizi ukilinganisha na siku za Yesu? ________________. Je! unajua kuhusu baadhi ya mateso yaliyoko siku hizi? Elezea: ____________________________________ ______________________________________________.
6. Soma Mathayo 7:7-12. Wale wenye kupata mateso lazima wadumishe mahusiano ya karibu sana na Baba yao wa Mbinguni. Mungu yupo tayari kuwapa wale ambao _________________. Je! wewe kama baba (mama) ungempa mwanao mwenye njaa jiwe au nyoka? __________. Je! unautumainia wema wa Baba yako aliye Mbinguni? ___________. Kulingana na mstari wa 12, ni nini muhtasari wa sheria na manabii? ______________________________________________.
7. Soma Mathayo 7:13-14. Yeye mwenye kuteseka na mateso yasiyo haki anaitumainia siku ile ambapo Mwamuzi Mkuu atahukumu mambo yote kwa usahihi. Inaonekana kuwa ni jambo geni, lakini katika njia ya wokovu kuna ___________________, lakini katika njia ipelekeayo upotevuni, kuna ______________________________. Kwa hiyo mwenye kuteswa anaweza kuwa na uhakika wa uzima wa milele, hata ingawa pote panapomzunguka kuna wengi wanaoelekea upotevuni.
8. Soma Mathayo 5:11-12. Wanafunzi wana heri na furaha wakati watu wanapowanena vibaya kwa uongo. Kulingana na mstari wa 12, wangeliitikiaje hilo? ______________________. Soma Mathayo 7:15-19 pia. Waongo wa kidini ni wale manabii wa uongo wenye kuvaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani ni ___________. Unawezaje kuelewa kama mti ni mzuri au la? _____________. Na unawezaje kumtambua nabii wa uongo? ____________________________.
9. Soma Mathayo 7:21-23. Aina nyingine ya mwongo ni yule mwenye kufanya kila kitu isipokuwa kuyatii mapenzi ya Mungu. Yeye angesema, Bwana, Bwana, akitoa uelewa kana kwamba yuko chini ya ubwana wa Kristo. Yeye hata angefanya maajabu makubwa katika jina lenye nguvu la Yesu. Je! ni makosa kutoa unabii, kutoa mapepo au kufanya miujiza? ____________. Hata hivyo, ni makosa, kufanya mambo katika jina la Kristo pasipo kukubali kuyafanya _______________ ya Baba aliye mbinguni.

10. Sasa soma kifungu cha mwisho cha Hotuba Mlimani katika Mathayo 7:24-29. Katika kifungu hiki tunauona uthibitisho wa mwanafunzi wa kweli. Mtu mwenye hekima ni yule mwenye kuyasikia haya mafundisho na kuya_____________________. Mtu mpumbavu ni yule mwenye kuyasikia haya maneno lakini haya _______________________________
____________________________________________________________.
Kilitokea nini katika nyumba ya mtu mwenye hekima? ______________.
Na katika nyumba ya mtu mpumbavu? ___________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Mwanafunzi anawezaje kuwa mpatanishi katika makazi, jamii na mataifa?

2. Je! tuna ujumbe wa amani kwa ajili ya mataifa?
Ni ujumbe gani?

3. Katika nyakati za nyuma pamekuwepo na miundo ya mateso ya fujo. Katika nyakati zetu mateso yanachukua muundo wa aina gani?

4. Mafundisho ya manabii wa uongo wa nyakati zetu ni yapi?

5. Matendo makuu ya Mungu ni mazuri, lakini uthibitisho wa mwanafunzi wa kweli ni nini?

# Somo la 7

## Kufanyiza kwa Mwanafunzi kwa Njia ya Mahusiano ya Kibinadamu

Lengo: Zigundue sifa za mitazamo ya mwanafunzi katika mahusiano yake na wengine

1. Mwanafunzi katika mpango wa mafunzo wa Yesu ilimpasa ajifunze kuishi pamoja na wengine. Yesu alikusanya watu kumi na wawili waliokuwa tofauti sana katika tabia zao na uelekeo. Petro alikuwa mwenye msukumo sana, na aliyaelezea maoni yake kwa mara moja. Yohana alikuwa mkimya zaidi, lakini alikuwa amejitoa sana kwa Bwana wake. Tomaso wakati wote alitaka sababu thabiti za kuwekea Imani yake juu ya msingi. Wanafunzi walikuwa kama maktaba ya mahusiano ya kibinadamu, ambamo watu, waliokuwa na tofauti mmoja na mwingine, iliwapasa kujifunza kuishi pamoja. Kwa nini unafikiri kuwa ilikuwa ni muhimu kwa wanafunzi kuishi na kufanya kazi pamoja? ________________________________ ____________________________________________________________.
2. Ilipasa wanafunzi wafanye kazi pamoja ili kupata mitazamo sahihi katika mahusiano yao na wengine. Walipokuwa wakisafiri kama kikundi pamoja na Yesu, kila mwanafunzi akawa anaunda mitazamo iliyokuwa ya Kikristo zaidi. Je! unakumbuka jinsi ambavyo wanafunzi walibishana kuhusu ni nani atakayekuwa mkuu kuliko wote katika ufalme wa Mungu? Yesu akawaambia lazima wawe na unyenyekevvu na urahisi wa mtoto ili kuwa mkuu mbinguni. Ufalme wa mbinguni umeundwa na walio "maskini wa roho." Ni mitazamo ipi iliyo ya muhimu (ya lazima zaidi) katika kuishi pamoja na wengine? ___________________________________.
3. Unyenyekevu ni wa muhimu katika kumtii Mungu na kuishi pamoja na wengine. Haikuwa rahisi kwa wanafunzi kujifunza unyenyekevu. Soma Mathayo 20:20-28. Hata mama yake wa wawili kati ya wanafunzi alitaka Yesu aamuru kwamba wanawe waketishwe, mmoja __________________ na mwingine ____________________ pamoja na __________________ wakati Yesu atakapofika katika ufalme wake. Wanafunzi wengine waliposikia hili, wali____________________ na ________. Yesu alielezea kuwa katika falme za duniani, walio wakuu hutumia mamlaka juu ya wengine, lakini kati ya wanafunzi, kanuni itakuwa: Yeyote atakayetaka kuwa mkuu kati yenu, ______________________________________.
4. Mwanafunzi huyu lazima awe mtumishi kwa sababu Yesu amekuja kutumikia na hata _______________ kwa ajili ya wengi. Yesu ni mfano bora wa mahusiano mazuri ya kibinadamu. Yeye aliishi katika kujitoa Nafsi Mwenyewe kwa wengine. Kiini cha upendo wa Kikristo ni kujitoa wewe mwenyewe kwa wengine. Kiini cha upendo ulimwenguni ni

kujipatia kitu fulani kwa ajili yako mwenyewe. Tangu mwanzo hadi mwisho, uanafunzi una upendo huu wa Kikristo. Mwanzoni, Petro aliziacha nyavu ili kumfuata Yesu, lakini hata hivyo mwishoni wa wakati wake pamoja na wanafunzi, Yesu alimuuliza Petro ikiwa alimpenda zaidi ya nyavu zake za uvuvi. Asili ya upendo kidunia ni nini? ______________. Asili ya upendo wa Kikristo ni nini? ______________________.

5. Upendo wa Kikristo si tu kiini cha kimawazo, lakini ni wa kiutendaji sana. Iliwapasa wanafunzi watendee kazi upendo kwa Bwana wao na kwa wengine. Upendo wa Kikristo uaminifu wake wa kwanza ni kwa Kristo. Mwanafunzi anatafuta kwanza ufalme wa Mungu. Soma Mathayo 19:27-29. Kumtii Kristo kunaweza kuna na maana ya kuacha mali na milki za familia, lakini Kristo anaahidi kwamba watu wa namna hiyo watapokea mara ____________. Kristo pia anaahidi kuwa wale waliomfuata wataketi ______________. Mtume Paulo amefundisha kuwa wale wenye kuteseka pamoja na Kristo pia _______________ pamoja na Yeye.
6. Ingawa mwanafunzi anakubali kuicha familia yake ili amfuate Bwana, hili halina maana kuwa mwanafunzi hayathamini mahusiano ya kibinadamu. Soma Mathayo 18:6-9. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mwangalifu sana asi_____________ walio wadogo (watoto). Walio wadogo, kulingana na Mathayo 18:5, inazungumzia watoto wenye kufuata mfano wa watu wazima. Mwanafunzi mwaminifu yeye atawashawishi watu zaidi kwa mfano wake zaidi kuliko hata kwa mafundisho yake. Mfano mzuri ni ushuhuda bora wa mwanafunzi, na ushuhuda mbaya wa mtu fulani mwenye kujifanya mwanafunzi ni mfano _______________.
7. Mwanafunzi ana wajibu wa kujaribu kuwarejesha wale waliopotea kutoka kwa Bwana. Soma Mathayo 18:10-14. Wakati ndugu anapoondoka kutoka katika njia ya uanafunzi, mara nyingi ni asilia kumhukumu kwa ukali. Lakini kulingana na mstari wa 12, mwanafunzi mwenye kufauata mfano wa Bwana wake ata____________ aliyepotea. Na atakapompata, atamkemea? _________________. Badala yake kuna ________________ zaidi juu yake kuliko wale na wale ambao hawakupotea.
8. Wanafunzi wanatakiwa kufurahi wakati ndugu aliyepotea anarudi katika njia ya uanafunzi. Hili linawezekana tu wakati wanafunzi wengine wamejifunza kusamehe. Soma Mathayo 18:15-19. Kuna hatua tatu za upatanisho zilizotajwa hapa. Ya kwanza ni kumwambia makosa yake, kuwa _____________________. Je! sisi huwa tunalitendea hili kazi? _________________. Je! mara nyingi zaidi huwa tunakwenda na kuwaambia wengine kuhusu hili? _________. Kama hatua ya kwanza haijafanikiwa, hapo tu ndipo tuchukue hatua ya pili ya kuchukua _________ wawe mashahidi. Kama asikii, hatua ya tatu ni kuliambia hilo kanisa. Kusudi la kuongea na ndugu ni nini-je ni kupatana naye au kumfukuza? ____________________________________________________ ____________________________________________________________.

9. Mwanafunzi anafanya kila kitu awezacho ili kuleta upatanisho, na ni pale tu wakati ameisha yafanya yote matatu pasipo kuyapata matokeo yaliyotarajiwa ndipo atamhesabu huyo ndugu hawezekani kupatanishwa na kwamba yu nje ya ushirika. Kusanyiko dogo sana linaweza kuufurahia uwepo wa Yesu. Soma Mathayo 18:20-22. Je! Yesu wakati wote yupo katika kusanyiko la wawili au watatu? ____________. Wanatakiwa kukusanyika katika ____________ la ______________. Hili lina maana kuwa kusanyiko la wanafunzi wanafikiri na kutenda wakifuata mfano wa Yesu. Yeye mwenye kuufuata mfano wa Yesu anakubali kusamehe hadi ____________ mara ________________.
10. Kusanyiko hili limeshiriki pia katika Chakula cha Bwana. Soma Mathayo 26:26-29. Meza hii ipo ili itukumbushe jinsi ambavyo Yesu alitunza maisha ya kijamii ya wanafunzi. Pia, Chakula hiki kinatangaza kuwa damu yake itamwangwa kwa ajili ya ondoleo la ______________. Kwa hiyo chakula cha mwisho kinaashiria mateso yake duniani, na kushinda kwake baadaye katika uwepo wa Mungu Baba.
11. Ni wazi kuwa Yesu alitamani uanafunzi uendelee kwa njia ya Ushirika wa Kikristo. Jamii ya Wakristo baadaye ilikua na kuwafikia watu wengi. Kwa hiyo hata ingawa kanisa letu linakua ni muhimu sana pawepo na mahusiano ya karibu ya makundi ya wawili au watatu wenye kukusanyika kwa jina lake. Je! kanisa la leo linawezaje kutunza ukaribu wa makundi madogo madogo? ________________________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Ni nini tofauti kati ya kuwa wakuu ulimwenguni na katika uanafunzi? Ni nini tofauti kati ya upendo wa ulimwengu na upendo wa Kristo?

2. Tunawezaje kushughulika na wale walioacha kumfuata Bwana katika uanafunzi?

3. Elezea kwa maneno yako mwenyewe njia ya matendo ya kupata uzoefu wa Mathayo 18:15-19. Makosa ya kawaida sana katika kulitenda hili ni yapi?

4. Faida za makundi madogo ya Wakristo ni zipi? Faida za ibada zinazohudhuriwa vizuri ni zipi?

## Somo la 8

## Mazoezi ya Uanafunzi Kulingana na Uhusiano na Ulimwengu

Lengo: Elewa mtazamo wa Yesu na Wanafunzi wake katika mahusiano na Ulimwengu.

1. Wanafunzi wa Yesu iliwapasa wajinze mengi kuhusu uhusiano wao na ulimwengu. Mwanzoni, mitazamo yao haikuwa mizuri. Soma Luka 9:51-56. Wakati watu hawakutaka kuwapokea, wanafunzi walitaka kufanya nini? ______________________________. Yesu aliwakemea kwa sababu hakuja kuangamiza maisha bali ku ______________________________.
2. Yesu pia alikula na wenye dhambi na watoza ushuru. Watu wa kidini walistajaabishwa na Matendo yake. Soma Mathayo 9:10-13. Yesu hakuja kuwaita wenye ___________________ bali wenye ____________________ watubu. Kama mtu huwatembelea watu walio wenye haki peke yake, hataweza kuwafikia wenye dhambi na Injili. Ili kuona wenye dhambi wanafikiwa na kuletwa kwa Bwana, ni muhimu ku ___________________ ________________________.
3. Yesu pia alishughulilka na viongozi wa kidini. Katika Mathayo 23 Yesu alionyesha unafiki wa wale walijifanya wanamtumikia Mungu. Soma Mathayo 23:1-3. Tatizo ni kwamba walisema, lakini ___________________, amri. Yesu aliwaita makaburi yaliyopakwa chokaa yaliyojaa mifupa ya wafu. Lakini ili kuelewa mtazamo wa Yesu, Soma Mathayo 23:37. Je! Yesu alitaka kuwahukumu au kuwaokoa? Moyo wa Yesu ulisikia upendo wa ukombozi kwa ajili ya hawa watu wa dini waliopotea, lakini uasi wao wenyewe ulikuwa umewaletea ukiwa katika nyumba zao.
4. Labda ungefikiri kuwa Yesu angezungumza vizuri na watu wa dini na kuwahukumu wenye dhambi, lakini katika matukio mbali mbali, Yesu aliwaonyesha huruma kubwa wenye dhambi waliokuja kwake Yeye. Kwa mfano soma Luka 7:36-37. Yesu alikuwa katika nyumba ya ______________________________. Lakini alikisifu zaidi kile alichokitenda mwanamke mwenye dhambi. Yesu aliweka wazi kuwa yeye aliyesamehewa kidogo hupenda kidogo; lakini yeye aliyesamehewa vingi hupenda sana ____________________________________.
5. Yesu hata alizitumia fursa alizokuwa nazo kuwashuhudia watawala wa serikali. Hata ingawa alijua kuwa Pilato atamtoa Yeye akasulubiwe, Yesu alimwambia mamlaka yote ya serikali yameruhusiwa na Mungu. Soma Yohana 19:11. Kwa namna hiyo hiyo, Yesu alitangaza katika Yohana 18:36 kwamba ufalme wake haukuwa wa ulimwengu huu, na kwa sababu hiyo, wafuasi wake wasingepigana. Yesu Mfalme alikubali kuteseka katika

mikono ya watawala wa ufalme wa dunia hii. Ikiwa Bwana anakubali kuteseka, mwanafunzi anatakiwa kuwa tayari ______________________.

6. Yesu alijaribu kuwafundisha wanafunzi wake kuhusu mateso. Mara kadha wa kadha alizungumza nao kuhusu mateso yatakayokuwepo baadaye. Wanafunzi walitumwa kama kondoo katikati ya mbwa mwitu wakali. (Mathayo 10:16) Petro hakutaka kuupokea ujumbe wa mateso. Soma Mathayo 16:21-24. Lakini mtazamo wa Petro haukuwa umevuviwa na Mungu, bali na ________________. Yesu alisema, Mtu ye yote akitaka kunifuata, ______________ mwenyewe, ajitwike ______________ wake, __________________. Je! unafikiri kuuchukua msalaba wako maana yake kuning'iniza msalaba kwenye shingo yako? ______________. Elezea. ____________________________________.
7. Ingawa mwanafunzi huuchukua msalaba wake wa mateso, hii haina maana kwamba atasahau uaminifu wake kwa Kristo Bwana wake. Wakati swali kuhusu kulipa kodi lilipoinuka, Yesu alionyesha tofauti kati ya falme mbili. Soma Mathayo 22:17-22. Tumpe nini Kaisari? _______________. Tumpe nini Mungu? ________________________________________.
8. Yesu alijibu swali la uangalifu sana kwa hekima. Katika kila zama ya historia, iliwapasa wanafunzi wajifunze ni nini yaliyo ya Kaisari, na ni nini yaliyo ya Mungu. Ni wazi kuwa Mungu ana shughuli fulani, na Kaisari anayo nyingine. Wanafunzi wakajifunza baadaye kuwa hata mamlaka za serikali zilitakiwa kujinyenyekeza kwa Mungu. (Warumi 13) Katika haya yote, mitume wakati wote uaminifu wao wa kwanza waliubakiza kwa Mungu. Lakini katika nyakati za mgogoro, wanafunzi walichagua njia ya mateso. Tufanye nini wakati watawala wanapotuagiza tufanya kitu fulani kilicho kinyume na mapenzi ya Mungu? __________________________ ________________________________________________________.
9. Yesu pia alifundisha kuhusu matukio kati ya mataifa katika wakati ujao. Soma Mathayo 24:3-14. Wanafunzi walitaka kujua ni nini kitatokea. Katika wakati ujao mataifa yatateseka na majanga mengi. Yaorodheshe majanga yaliyotajwa katika mistari wa 6 na wa 7. ___________________. Lakini pia patakuwepo na kazi za kiinjilisti. Kulingana na mstari wa 14, Tena ________________________________________________ itahubiriwa ________________________, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule __________________ utakapokuja.
10. Kwa namna hiyo Yesu alitabiri kuhubiriwa kwa habari njema za ufalme katika ulimwengu wote. Mwanafunzi yuko ulimwenguni ili ashuhudie ulimwenguni. Hata maneno ya mwisho ya Bwana Yesu yalionyesha agizo la umisheni kwa ulimwengu. Soma Mathayo 28:18-20. Ni nani aliye na uweza wote ulimwenguni? ______________________. Kwa sababu hii wanafunzi wanatakiwa kwenda na __________________________ kwa ______________________ yote.

11. Mataifa ya ulimwengu yanatakiwa kuwa ndiyo walengwa wa agizo la kufanya wanafunzi. Katika ulimwengu wenye uhasama, mwanafunzi aliyejitakasa anahubiri injili ya ufalme ili afanye wanafunzi zaidi. Katika agizo la Yesu, kuna maneno kadha wa kadha ya kutenda. Basi, ____________________, ________________________ mataifa yote kuwa wanafunzi, ________________________ kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Pia, wanafunzi walitakiwa ________________ kuyashika yote aliyoyaamuru Yesu. Wakati wanafunzi wanafanya hili, Yesu anaahidi kuwa pamoja nao hata _________________ wa ________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Wanafunzi walikuwa wakifanya kosa gani walipotaka kuita moto juu ya wale walioyapinga mahubiri yao ya injili?

2. Kwa nini unafikiri kuwa Yesu alihusika kwa ukali sana na viongozi wa kidini na kwa upole sana na wenye dhambi waliokuwa wanajulikana?

3. Tunaweza kufanya nini kama wanafunzi wa Yesu wakati watawala wa serikali wanapotuamuru kufanya yale yaliyo kinyume na mapenzi ya Mungu?

4. Ni agizo gani aliloliacha Yesu kwa wanafunzi la kwenda katika mataifa?

## Somo la 9

## Uzazi na Kufanyiza/Malezi ya Wanafunzi

Lengo: Onyesha hatua alizozichukua Yesu ili kumfanya kila mwanafunzi kuzaa matunda.

1. Tangu wakati ambapo Yesu aliwachagua wanafunzi wake, kusudi lake lilikuwa wazi. Utakumbuka wakati Yesu aliposema, Nifuate nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. Maneno "nifuate," yaliyonenwa na Yesu yananena juu ya kufanyika mwanafunzi kwa njia ya kuwa katika uwepo wa Yesu, kuyasikia mafundisho yake na kuwa na uhusiano na Yesu. Katika maneno machache ya kauli hii, Yesu alisema atawafanya wawe wavuvi wa watu. Kuwa wavuvi wa watu ina maana kufanya wanafunzi wengine, uzalishaji. Kwa kuelezea kifupi, Yesu alikuwa akiwafanya wanafunzi ili waweze kufanya wanafunzi wengine. Nini kingitokea kama mtu asiye na mafunzo angejaribu kufanya wanafunzi? ________________ ______________________________________________________________.
2. Kwa asili angekuwa na hali ya kufanya mwanafunzi mwingine ambaye hajapewa mafunzo. Inawezekana katika nyakati zingine kwa mwanafunzi mwenye taarifa kidogo, kwa neema ya Mungu, kuzaa mwanafunzi aliyetengenezeka vizuri. Lakini kwa ujumla, mwanafunzi atazaa mwanafunzi mwingine kama yeye mwenyewe zaidi au pungufu. Kuna wale wanaofikiri juu ya uanafunzi tu kama mfanyizo/malezi au mafunzo, bila kufikiria uzazi. Watu wa namna hiyo wako fasaha katika ufafanuzi wao wa utii, msalaba, na gharama ya uanafunzi, lakini hawaneni lolote juu ya umuhimu wa kuzaa. Nini kingetokea kama tungeweka jitihada zetu zote katika kufanywa kwa wanafunzi na tusiweke jitihada yeyote katika kuzaa wanafunzi? ____________________________________________.
3. Kwa asili, matokeo yangekuwa kwamba baada ya muda hapatakuwa na wanafunzi tena kwa sababu wale wanafunzi waliopewa mafunzo vyema wangekufa, na kama hawakujidhalisha wenyewe ndani ya wengine, hapatakuwepo na wanafunzi tena. Lakini pasiwepo pingamizi kati ya mfanyizo/malezi na kuzaa. Kama mwanafunzi amefanywa kuwa mfuasi wa Yesu kweli kweli, kiasili atafanya wanafunzi wapya. Pia, kama mwanafunzi anataka kuzaa wanafunzi wa kweli, yeye mwenyewe lazima awe mwanafunzi mwaminifu wa Bwana Yesu Kristo. Kwa maneno fasaha, kuwa mwanafunzi maana yake kufanya wanafunzi. Mwanafunzi aliyekomaa anatakiwa ____________________ wanafunzi wapya, na ili kufanya hili anatakiwa kuwa ____________________________________.
4. Sasa hili halina maana kwamba mwanafunzi lazima asubiri hadi mfanyizo/malezi kwake kumemalizika ndipo afanye wanafunzi kwa ajili ya Yesu. Kufanyika kwetu hakutakuwa timilifu mpaka Kristo

atakapodhihirishwa (1 Yohana 3:2). Badala yake, mwanafunzi anajizalisha mwenyewe wakati wote wakati yeye mwenyewe anafundishwa na anafanyizwa. Hebu tutazame baadhi ya mifano. kulingana na Yohana 1, Andrea alianza kumfuata Yesu, na muda mfupi sana baada ya hapo, akamleta ndugu yake Petro kwa Yesu. Soma Mathayo 10:1, 7. Wakati wanafunzi wa kwanza wanapewa mafunzo, walikuwa wakiwashuhudia wengine. Sehemu ya mafunzo yao na malezi ni kutoka na kuhubiri. Njia moja ambayo kwa hiyo mwanafunzi anaweza kuendelea katika mfanyizo/malezi wake ni ipi? ____________________________________
______________________________________________________________.

5. Kushiriki kwao katika safari zao za kiinjilisti kuliwasaidia kuwa wanafunzi bora. Tunaweza kuona kwamba kama wanafunzi wangeiacha kazi ya uinjilisti, tusingejua lolote kuhusu injili ya ufalme wa Mungu leo. Ni wazi kwetu kuwa mfanyizo/malezi na uzaaji havitengani. Kumbuka agizo la Bwana katika Mathayo 28. Lazima tufanye wanafunzi, lakini kazi ya kufanya wanafunzi inajumuisha jukumu la kuwafundisha yote aliyoyafundisha Yesu. Mara nyingi kuna makanisa ambayo ni dhaifu waeuweka uinjilisti juu ya kila kitu kingine na wamefeli kufundisha uanafunzi. Je! kusanyiko lako linaonyesha ishara ya tatizo hili? __________. Elezea ______________________________________________________.
6. Sasa tutayaangalia maelekezo aliyoyatoa Yesu kuhusu kuzaa wanafunzi. Soma Mathayo 10:5-6. Yesu aliwatuma kwanza kwa Wayahudi. Wanafunzi pia walikuwa wayahudi. Mwanafunzi anatakiwa kuanza kufanya wanafunzi kati ya watu wake mwenyewe. Wakati wote kuna mtu fulani ambaye tuna mawasiliano ya namna fulani na yeye. Kumbuka jinsi ambavyo Andrea alimleta ndugu yake mwenyewe. Una familia na marafiki. Ni kina nani kati ya familia na marafiki sio wanafunzi wa Yesu? ________________________. Basi hapo unatakiwa kufanya nini? _________________________________.
7. Unaweza kuwafanya kuwa wanafunzi watu hawa ambao una mawasiliano nao. Lazima usifikiri kuwa ni mchungaji peke yake au mhubiri ndiyo wanahitaji kufanya hivyo. Soma Mathayo 10:11. Kwa njia hii, familia katika mji ilijitambulisha pamoja na Injili, na ikaiwakilisha Injili hata baada ya mwanafunzi kuondoka na kwenda maeneo mengine. Je! unayajua makanisa yalioanza katika nyumba? _________________________. Wakati mwingine kanisa linakua na hatutakiwi kusubiri hadi watu waweze kwenda hekaluni. Je! tufanye nini wakati kazi inapoendelea kukua? ______ ______________________________________________________________.
8. Kuna hoja nyingine muhimu katika maelekezo ya Yesu. Soma Mathayo 10:14. Kama baadhi hawataki kupokea ujumbe wetu, tufanye nini? ______________________________. Tunatakiwa tufikiri juu ya faida za haya maelekezo. Kwa njia hiyo wanafunzi wangeweza kuutoa muda wao kwa watu wenye kupokea. Yesu hakutuagiza tufanye kazi pasipo kuona

matokeo yeyote. Lakini kama ambavyo tumetaja kabla, wanafunzi wanaweza kuwa walengwa wa mateso. Soma Mathayo 10:16. Wanafunzi wanatakiwa kuwa wenye hekima kama ________________________ na wapole kama ________________________.

9. Kuna wakati ambapo injili inaleta matengano. Soma Mathayo 10:34-39. Injili ya ufalme ni yenye kuleta mapinduzi, na yeye mwenye kumpenda baba au mama zaidi ya anavyompenda Yesu yeye si ______________________________ wa Yesu. Kujitwika msalaba ina maana kumpenda Yesu sana na juu ya mengine yote, na Kuyafanya mambo mengine yote kuwa ya pili. Uzima wa milele una thamani kubwa kuliko zote. Ni nani mwenye kuokoa/kuponya maisha yake? Ni nani mwenye kuyapoteza maisha/nafsi yake? ____________________________.
10. Lazima tuutambue umuhimu na thamani ya uanafunzi. Soma Mathayo 10:40-42. Mwanafunzi mwaminifu ni mwakilishi wa Kristo. Wale wenye kumpokea mwanafunzi wanampokea ______________________________. Hata kumpa kikombe cha maji ya baridi mwanafunzi hakutapoteza _________________ yake. Kutumika kama mwakilishi wa Yesu ni wasaa mkuu na usichukuliwe kwa wepesi. Hili lingeonekana kusema kwamba kama familia imempokea mwanafunzi nyumbani kwao, ingetarajiwa kuwa hii familia wangekuwa wanafunzi. Kuna nyumba ngapi zilizo wazi kwa wewe kuzitembelea? ____________________. Je! umeanza kuzifanya hizi familia kuwa wanafunzi? ____________________.
11. Hata ingawa si nyumba zote ziko tayari kuwa wanafunzi, kuna miji na vijiji ambavyo viko tayari kuupokea ujumbe huu. Soma Mathayo 13:1-9. Si udongo wote huzaa matunda. Lakini, kulikuwepo na udongo ambao ulizaa matunda, ________________, na baadhi _______________ na baadhi _________________. Mkulima mzuri anapanda zaidi na anavuna zaidi kutoka katika udongo wenye rutuba. Kuhusu miji na vijiji ambavyo unajua kuhusu hivyo, ni vipi ambavyo vinapokea injili? ____________________________. Kati ya watu unaowajua, ni wapi wenye kupokea zaidi? ________________________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Je! ni jambo lenye afya kwa kusanyiko kama mchungaji anazungumza tu kuhusu utii na kuuchukua msalaba ili kumfuata Kristo? Kikosekanacho ni nini?

2. Kila mwanafunzi aanze kufanya uinjilisti wapi? Kwa nini?

3. Je! ni hekima kuwahubiri watu wenye kuikataa Injili? Kwa nini unajibu kwa njia hii?

## Somo la 10

## Uzazi wa Wanafunzi

Lengo: Jifunze zaidi kuhusu hatua alizozichukua Yesu ili kuwaendeleza wanafunzi kwa njia hii.

1. Katika somo lililopita, umeanza kujifunza mfano wa mpanzi na mbegu na aina nne za udongo. Sasa soma tafsiri ya mfano huu katika Mathayo 13:18-23. Tengeneza orodha ya matokeo ya kupanda katika aina tofauti za udongo, ukizilinganisha na mitazamo ya watu.
   –Zilizopandwa kando ya njia - alisikiapo ____________________ la ufalme ________________ nalo.
   –Zilizopandwa penye miamba - yeye mwenye kulipokea Neno kwa ____________________ lakini hana ________________ndani yake, bali ________________________ kwa muda.
   –Zilizopandwa penye miiba – na ____________________ za dunia hii na _________________________ wa mali ____________________ lile Neno.
   –Zilizopandea penye ugongo mzuri - huyo ndiye ____________________ lile Neno na ____________________ nalo; yeye ndiye azaaye ______________________________________.
   Mpanzi wa Neno la Mungu mwenye hekima anatakiwa kujua jinsi ya kuuchanganua udongo anaoupanda. Tunatakiwa kupanda na kupalilia zaidi wapi? ____________________________________________________.
2. Mfano wa ngano na magugu katika Mathayo 13:24-30 unatufundisha sisi kwamba ufalme wa Mungu upo katika ulimwengu wa uovu hadi siku ya hukumu ya mwisho ambapo magugu yatachomwa moto. Soma Mathayo 13:31-33. Hapa kuna mifano miwili kuhusu ukuaji. Mbegu ndogo sana ya haradali inakua na kuwa ______________________________. Kwa hiyo kundi dogo la wanafunzi wenye kuzaa wanaweza kukua na kuwa kundi kubwa la wanafunzi. Pia, katika mstari 33, tunaona athari ya chachu. Karibia wakati wote katika Biblia, chachu maana yake ushawishi mbaya. (Tazama Mathayo 16:5.) Hili linaashiria ushawishi mbaya utaongezeka katika wakati ujao. Maana ya unabii alioutoa Yesu katika Mathayo 24 ni kwamba mgogoro kati ya mabaya na mema utaongezeka sana katika wakati ujao. Katika Biblia chachu ina maana gani? ____________________ ______________________________________________________________.
3. Thamani ya Ufalme wa Mungu inaonyeshwa katika mifano miwili. Soma Mathayo 13:44-46. Yule mtu aliyeipata hazima alifanya nini? _________________________________. Mfanya biashara aliyepata lulu ya gharama kubwa alifanya nini? ______________________________________. Katika matukio mbali mbali Yesu alinena kuhusu thamani ya uanafunzi.

Tufanye nini tunapoupata uzima wa milele? ______________________
______________________________________________.

4. Hatuna nafasi hapa ya kuonyesha mafundisho yote ya mifano ya Yesu. Lakini mafundisho makuu yako wazi. Kazi ya Mungu itakua, lakini Itakua katikati ya maovu yanayoongezeka; na pamoja na kuwepo mgogoro kati ya mema na mabaya, wakati wote gharama inastahili ya kumfuata Yesu. Hili linathibitishwa na mafundisho yake mengine kuhusu gharama ya uanafunzi. Thamani ya uanafunzi ni kwamba wanafunzi wana wajibu wa kuwashirikisha wengine maisha yao. Yote haya yanatufundisha sisi kitu fulani kizuri na kitu fulani kibaya. Kizuri ni kuwa tujitahidi kwa ajili ya ukuaji wa kazi ya Mungu, na upande mbaya ni kuwa lazima tuwe na uelewa wa uhalisi kuwa uovu utaongezeka pia. Wajibu wa Mkristo ni nini katika kuikabili hali hii? ______________________________
______________________________________________.
5. Yote haya yanaashiria kuwa lazima tuwe na nguvu ya Mungu ili tushinde. Soma Mathayo 16:15-18. Petro alikiri kwamba Yesu ni ______________, ____________________ wa Mungu ______________________. Ukiri huu unatengeneza msingi wa imani kwa ajili ya wanafunzi wa zama zote. Mungu anawatumia wanafunzi wake kulijenga ____________________ na malango ya ________________ hayata__________________. Hili ni kanisa lenye kuzishinda nguvu zote za uovu. Yesu hakuwa anamsifu Petro kwa kulisema hili, au hakuwa anasema angelijenga kanisa lake juu ya Petro. Katika Mathayo 16:23, Petro alitumika kama mjumbe wa Shetani, na katika nyaraka alizoziandika Petro, anatangaza wazi kuwa jiwe kuu la pembeni ni Yesu. (1 Petro 2:4-6) Lakini kila mwamini ni jiwe lililo hai. (Tunapozungumza juu ya kanisa, wakati wote tusifikiri juu ya kanisa lenye kuonekana kwa macho la leo kuwa ndiyo lazima ndiyo ufalme wa Mungu.)
6. Kwa hiyo kanisa linalojengwa juu ya Kristo, lakini lililofanywa na wanafunzi wake, litakuwa lenye kushinda katikati ya dunia yenye uhasama. Kazi hii isingekuwa yenye kuwezekana pasipo msaada wa Roho Mtakatifu. Soma Yohana 14:16-17. Mfariji atakuwa pamoja na wanafunzi ______________________. Yesu alisema wanafunzi, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, wangezifanya kazi alizozifanya Yesu, naam, na ____________ ________________ hizo atazifanya. (Tazama Yohana 14:12.)
7. Lakini ili kuweza kuzaa matunda zaidi, lazima tudumishe mahusiano ya karibu sana na Yesu. Soma Yohana 15:1-5. Ni nani aliye mzabibu? __________________. Kina nani ni matawi? ____________________. Matunda yanazalishwaje? ________________________________. Mwanafunzi anaweza kuendelea kuzaa matunda kama tu anaendelea kuwa katika muunganiko na Bwana Yesu Kristo, Mzabibu wa kweli. Mwamini mwenye kuyumba-yumba katika uaminifu wake hatazaa matunda mengi. Badala yake itabidi ndugu wachukue muda mwingi wa kumtia moyo, na

hataweza kuutoa muda mwingi kwa waamini wapya na katika uinjilisti. Fikiri kuhusu hili. Je! wewe ni mwanafunzi mwenye kukaa kwa kudumu katika Kristo, na kwa sababu hiyo unazaa matunda? ________________. Kama siyo, fikiri kuhusu yale unayoweza kufanya.

8. Matunda ambayo Mungu anayatamani ni ya namna-mbili. Kwanza, tunda la Roho ndani mwetu, (Wagalatia 5:22-23). Halafu uzaaji wa wanafunzi wapya. Yesu alijua kuendelea kwa kazi yake kutategemea yale ambayo Mungu atayafanya kupitia wanafunzi wake ambao wamefanya wanafunzi wengine. Aliona mashamba yameiva tayari kwa ajili ya mavuno. Soma Mathayo 9:36-38. Mavuno yako ______________________________ lakini ________________ ni ____________. Ufumbuzi wa hili ni nini? ______________________. Tunatakiwa tuombe kwamba Mungu atume/apeleke watenda kazi. Lakini atawatuma nani?
9. Yesu aliwatuma wanafunzi wake. Soma Yohana 20:21-22. Kama Baba ______________ mimi, nami _________________ ninyi. Ni nani atakayetumwa? ______________________________. Kama wewe ni mwanafunzi wa Yesu, wewe ni mwanafunzi aliyetumwa/ aliyepelekwa. Katika tukio hili hili, Yesu aliwaambia umuhimu wa kumpokea Roho Mtakatifu.
10. Ni kwa msaada wa Roho Mtakatifu peke yake ndiyo iliwezekana kwa wanafunzi kuendeleza kazi ya Kristo. Soma Luka 24:49. Walitakiwa kukaa Yerusalemu mpaka wakati gani? __________________________. Nini kingetokea kama wanafunzi wangejaribu kuifanya kazi ya Bwana pasipo nguvu ya Roho Mtakatifu? __________________________. Maneno haya ya mwisho ya Yesu ni muhimu sana kwa sababu yenyewe ni kiungo ambacho kinaiunganisha huduma ya Yesu na kazi ya mitume katika Kitabu cha Mitume. Soma Matendo 1:4-8. Wanafunzi walisubiri katika maombi kwa ajili ya kutimizwa kwa ahadi aliyowapa Yesu. Katika siku ya Pentekosti, walipokea nguvu wawe mashahidi katika _______________, na katika _____________ na __________, na hata katika __________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Katika mifano ya Yesu kuhusu “hazina” na “lulu ya thamani kubwa,” unafikiri hii ina maana gani?

2. Ni nani aliye jiwe kuu la pembeni la kanisa? Ni kina nani ndiyo mawe mengine yaliyo hai katika nyumba hii ya kiroho (kanisa)?

3. Ni nini hutokea kwa tawi (mwanafunzi) ambaye hazai matunda?

4. Iliwapasa wanafunzi wafanye nini ili wapokee nguvu? Basi, sisi yatupasa tufanye nini ili tuwe na nguvu ya kuwa mashahidi?

# Somo la 11

## Kanisa Ni Nini?

Watu wengi wana mawazo ya kuwa kanisa ni nini. Baadhi ya mawazo haya ni sahihi, lakini mengine si sahihi. Ni muhimu kuona Biblia inasemaje kuhusu kanisa.

### I. Yale Ambayo Watu Wengi Wanafikiri:

1. Watu wengi wanafikiri kuwa kanisa ni jengo. Kanisa kuu au hekalu lenye kushawishi lenye kuwavutia kutazama. Kwa hiyo kuna viwango vikubwa vya hela zinazowekezwa katika majengo ya kidini ya jinsi hiyo. Angalau jengo linabaki kama ukumbusho wa jitihada za mjenzi wake. Je! unafikiri kanisa ni kitu cha kuonekana kwa macho kama vile jengo? ____________.
2. Baadhi ya watu wanafikiri kuwa kanisa ni lililo na kundi la viongozi wa kidini. Wanapozungumza kuhusu kanisa, wanafikiri kuhusu watumishi, makuhani, maaskofu, wachungaji na mashemasi. Halafu wakati viongozi hawa hawatendi kama wanavyotakiwa, ni rahisi kushutumu na kusema, "Kanisa limekufa," au "Mimi sipendi kile ambacho kanisa linafanya." Je! wewe unafikiri kanisa ni kundi la viongozi wa kidini? ________________. Toa sababu ya jibu lako. ________________.
3. Halafu kuna wale wenye kufikiri kanisa kuwa ni Klabu ya Jamii. Watu wanakutana humo wanalifikiria kanisa ni utendaji wa kijamii tu. Kwa hiyo watu lazima wapewe burudani na kupendezeshwa. Na watu wanaenda wakitarajia kupokea kitu fulani ambacho kitakuwa cha kupendeza kupitisha wakati. Wakati halitimilizi yale waliyoyatarajia kwa namna hiyo, wanaacha kuhudhuria. Je! unaamini kwamba kanisa linatakiwa kukutana na mahitaji ya kijamii ya watu wake? ______________. Je! unaamini kanisa ni utendaji wa kijamii tu? _______________.
4. Matokeo ya mawazo haya yote, wengi wanafikiria kanisa ni mahali pa kuwatazama wengine. Wanaweza kulitazama jengo na kutoa maoni kuhusu hilo. Wanaweza kuwaona na kuwasikia viongozi, na kutoa maoni yao kuhusu je! wanayafanya yale wanayotakiwa kuyafanya. Pia, wanaweza kumchunguza kila mwingine ili waweze kusema je! huyu anapendeza, au mwingine hawavutii. Je! ni kweli kuwa kanisa la Yesu Kristo lipo ili tuweze kuwa wenye kutazamana? _________________. Sasa, kanisa ni nini, kulingana na namna yako ya kufikiri? ______________________________ ______________________________________________________.

### II. Biblia Inasemaje:

1. Biblia haifundishi kuwa kanisa ni jengo, lakini inafundisha li kama jengo. Mara nyingi kanisa la kwanza halikuwa na jengo maalumu la kukutania.

Mara nyingi kanisa lilikutana katika nyumba, katika mashule au nje katika uwanja. Hata hivyo, mtume Paulo analilinganisha kanisa na jengo. Kulingana na 1 Wakorintho 3:11, msingi wa kanisa ni ______________________. Pia, kulingana na 1 Petro 2:5, wafuasi wa Kristo ni kama mawe yaliyo hai ambayo yanatakiwa kujengwa kama ________ ___ ______. Kwa hiyo, kanisa _____ jengo, bali ni jengo la ______ yaliyo hai.

2. Wala Biblia haifundishi kuwa kanisa ni kundi la viongozi wa kidini, lakini ni kundi la watu wenye kujiunga ili kumwabudu na kumtumikia Mungu. Kama ambavyo tunasoma 1 Petro 2:9, Kanisa ni mzao mteule, ___________ wa kifalme, taifa _________, watu _____ _______________ _____ Mungu, walioitwa ______________ fadhili zake Yeye aliyetuita sisi kutoka ________ na kuingia katika __________. Kwa hiyo, tunaona kanisa si la kina makasisi, bali ni ukuhani ambao unjumuisha watu wote wa Mungu.
3. Biblia haifundishi kuwa kanisa ni klabu ya kijamii, lakini kanisa lina sehemu ya kijamii. Kulingana na Waefeso 2:19, sisi ambao ni wa kanisa tu washiriki/watu wa ___________________ mwa Mungu. Mara nyingi baba wa familia anaanza kanisa katika nyumba yake na watu wa nyumbani mwake mwenyewe. Paulo alituma salamu katika kanisa lilikutana katika nyumba ya Priska na Akila. (Warumi 16:5) Kuendelea kwa injili hakukuwa na haja ya kusubiri ujenzi wa majengo yenye gharama kwa sababu kwa sehemu kubwa kanisa lilikutana katika nyumba. Pia, kanisa la "familia" liliyashughulikia mahitaji ya washirika. (Wagalatia 6:10) Je! unaamini injili itakua kwa kasi zaidi kwa kutumia nyumba kwa nyumba kama sehemu za kukutania? ___________________________________________________.
4. Kwa nyongeza, Biblia inatufundisha sisi kwamba kanisa ni Bibi Arusi wa Kristo. Ndoa ni mahusiano ya karibu sana kuliko mahusiano yote ya binadamu. Soma Waefeso 5:25-27. Waume wanatakiwa kuwapenda wake zao, kama _______________ alivyolipenda ____________, _____________ kwa ajili yake; ili makusudi ________________ na _________________kwa maji katika __________; apate kujiletea Kanisa ______________, lisilo na______________ wala __________________. Katika kitabu cha Ufunuo karamu ya Arusi ya Mwana Kondoo imetajwa, wakati kanisa ambalo limekuwa mwaminifu litaungana na Kristo milele. Kwa hiyo tunaona kanisa sio Klabu ya Jamii, bali ni familia ya Mungu, hata ni Bibi Arusi wa Kristo.
5. Biblia haifundishi kuwa kanisa ni mahali ambapo tunatazamana sisi kwa sisi, lakini ni mahali pa maingiliano ya kimahusiano kati ya wote. Moja ya maelezo bora ya kanisa ni kuwa ni mwili wa Kristo. Wakolosai 1:18 inatwambia sisi kuwa Kristo ndiye__________cha mwili, yaani, cha ______________ … ili kwamba awe ___________________katika yote. Pia, Warumi 12:5 inasema kwamba ingawa sisi tu wengi, tu mwili mmoja, na _______________ kila mmoja kwa mwenzake. Katika 1 Wakorintho 12:12 Paulo anatumia mwili wa mwanadamu kama mfano: Maana kama

vile mwili ___________, nao una viungo vingi… hivyo na Kristo. Kwa hiyo inatarajiwa kuwa kila kiungo kitashiriki katika utendaji wa mwilil. Kwa namna hiyo hiyo, viungo vya kanisa hawatakiwi kuwa watazamaji bali washiriki.

**III. Muhtasari**

Wengi wanafikiri kuwa kanisa ni: jengo, wahudumu ambao ni viongozi wa kidini, klabu ya kijamii au mahali pa kuwatazama wengine. Lakini Biblia inatufundisha sisi kuwa kanisa ni kama jengo la kiroho lenye Kristo kama msingi, na wafuasi wa Kristo kama mawe yaliyo hai katika kuta. Pia inatufundisha kuwa viungo/washirika wa kanisa wanafanya ukuhani wa kifalme ili kumwabudu Mungu na kumtangaza Kristo ulimwenguni. Kanisa lina sehemu ya kijamii kwa kuwa ni familia ya Mungu, na ni Bibi-Arusi wa Kristo ambaye anatakaswa na kufanywa kuwa tayari kwa ajili ya Karamu ya Arusi ya Mwana Kondoo. Mwisho, kanisa ni mwili wa Kristo, wenye Kristo kama Kichwa, na wenye kila kiungo kinatenda kazi na kikiwa na umoja na viungo vingine.

## Utendaji wa Kikundi

1. Muwe na ubao karibu. Washiriki tofauti wa darasa waweze kuchora viwakilishi vya kanisa kwa picha, kama vile jengo, familia, kama mtu mume na mtu mke wenye mahusiano na mwili wa kibinadamu. Jaribu kuonyesha maana ya kila sehemu ya picha.

2. Sifa za kanisa liliratibiwa na kuelekezwa na mawazo ya kibinadamu ni zipi? Na zile za Kanisa lenye kuelekezwa na Kristo kama Kichwa ni zipi?

3. Je! unaamini kuwa kanisa linatakiwa kuimarishwa katika nyumba kwa nyumba katika jamii yako? Je! ni familia zipi ambazo unazijua ambazo ungekuwa tayari kuzitembelea?

# Somo la 12

## Sifa Za Kanisa

YUmejifunza kuwa kanisa ni kama jengo, ukuhani, ni familia, bibi-arusi na mwili. Katika somo hili, tafuta maana ya mifano hii. Kwa maneno mengine, tunajifunza sifa za kanisa.

### I. Sifa za Kanisa kama Jengo

1. Unakumbuka kwamba msingi wa kanisa ni Kristo, na viungo vyake ni kama mawe yaliyo hai. Tunahitaji kuchunguza zaidi maana ya mfano huu. Soma 1 Wakorintho 3:11-13. Jengo zuri linahitaji kujengea na malighafi zilizo bora. Katika mstari wa 12, tunaona kuwa kuna malighafi zenye kudumu kama vile __________________, ___________________ na mawe _________________. Malighafi nzuri ni zile ambazo zinaweza kustahimili kipimo cha moto. Kama viungo/washirika wa kanisa ni mawe yaliyo hai katika jengo hili, inaonekana Paulo anamaanisha kuwa kuna waamini ambao si malighafi zenye kudumu. Vipimo vinapokuja, hawadumu. Je! unawajua waamini ambao hawajamfuata Bwana kwa uaminifu? _____________. Wanatakiwa kufanyiwa nini? _________ ____________________________________________________________.
2. Makanisa mengi yamekuwa na washirika ambao hawakuendelea kwa uaminifu. Labda wamefeli kwa sababu walikuwa na dhana ya kimakosa ya kuwa kanisa ni kitu gani. Baadhi wameondoka wakiwa wameacha kumtazama Kristo kama Kichwa cha Kanisa, na wakaanza kuyaangalia mapungufu ya viongozi wa kanisa. Baadhi wamefikiri kwamba kanisa ni mahali tu pa kupokea baraka za kiroho na faida za vitu, lakini wamesahau kwamba kila kiungo/mshirika anatakiwa kutumikia katika kanisa. Kwa hiyo unaona tunahitaji kuwaelewesha vizuri zaidi ili waweze kuwa viungo/washirika wenye kudumu. Pia, soma 1 Wakorintho 3:16-17. Hekali la Mungu linatakiwa kuwa maskani ya _____________________________. Kwa hiyo hatutakiwi tu kumpokea Bwana, bali tunatakiwa kumpa Yeye maskani katika mioyo yetu. Ni nini tofauti kati ya watu ambao wanatarajia tu kupokea na wale wenye utayari wa kutoa? _________________________.

.

### II. Sifa za Kanisa kama Ukuhani

1. Tumejifunza kutoka katika 1 Petro 2:9 kwamba kanisa ni ukuhani. Kuhani ni yeye mwenye kuingia katika uwepo wa Mungu ili kupatana na Mungu na kumwabudu na kumtumikia Mungu. Katika Agano la Kale, ukuhani ulikuwa kati ya kundi lililochaguliwa, lakini sasa Yesu amempa kila mtu njia ya kufika katika uwepo wa Mungu. Je! kanisa ligawanywe kati ya makasisi na watu wa kawaida? __________. Ni kina nani ndiyo wanafanya kanisa? _____________.

2. Makuhani walitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zao wenyewe na pia kwa ajili ya dhambi za watu. Petro anatwambia kuwa tunatakiwa kuzitangaze sifa za Kristo kwa watu wote wengine. Washirika wengi wa kanisa hawafikiri juu ya huduma yao ya kikuhani kwa watu ambao bado wako nje ya kanisa. Kila mshirika wa kanisa anaweza kuwa kuhani katika jamii yake kwa njia ipi? ________________ ________________________________________________________________.

### III. Sifa za Kanisa kama Familia

1. Mtu anakuwa sehemu ya familia yaweza kuwa kwa njia ya kuzaliwa au kwa kufanywa mwana. Biblia inafundisha ili uwe sehemu ya familia ya Mungu lazima ______________________________. (Yohana 3:7) Pia, katika sehemu zingine katika Biblia tunaambiwa kuwa tumefanywa kuwa wana katika familia ya Mungu. Watu wengi hurudia kile ambacho huwa tunakiita Sala ya Bwana, au Baba yetu, lazima tuwe wana wake. Soma Yohana 1:12. Ni kina nani wenye haki ya kuwa wana wa Mungu, au watu wa familia yake? Wale ambao __________ Yeye, na ___________ jina lake. Kwa hiyo kanisa ni lenye watu waliozaliwa mara ya pili.
2. Watu waliozaliwa na baba mmoja ni ndugu. Kwa sababu hii, kanisa ni wana-ndugu. Soma Wagalatia 6:10. Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na ______________________; na hasa _____________ ya waaminio. Wakristo wanatakiwa kusaidiana kwa njia gani? ___________________.

### IV. Sifa za Kanisa kama Bibi Arusi wa Kristo

1. Paulo anatwambia kuwa kanisa ni Bibi Arusi Wake. (Waefeso 5:25-27) Kristo analipenda kanisa na anataka kulitakasa. Leo inaonekana kuwa ni ngumu kupata makanisa mengi yaliyotakaswa, lakini wakati huo huo Kristo anawasafisha watu ambao watakuwa sehemu ya kanisa Lake tukufu. Yesu ni Mwana Kondoo wa Mungu na yuko tayari kuzichukua dhambi ____________________. (Yohana 1:29) Soma Ufunuo 19:7. Siku itakuja ya ______________ ya Mwana Kondoo, na ______________ Wake amejitayarisha. Soma mstari wa 2 wa sura hiyo hiyo. Kinyume cha bibi-arusi aliyejitayarisha ni kahaba. Panasema kuwa ______________ mkuu ameiharibu nchi kwa ___________________________ wake. Kahaba ni kanisa lisilo mwaminifu ambalo linafanya dhambi na wafalme wa dunia. (Ufunuo 17:1-2) Kulingana na Biblia, katika siku za mwisho kutakuwepo na kanisa lililo mwaminifu ambalo Kristo atalipokea kama bibi-arusi Wake, na kanisa lisilo mwaminifu hilo litakuwa kama kahaba mwenye kuwapenda wafalme wa dunia hii. Kanisa lililo mwaminifu litakuwa __________ na kanisa lisilo mwaminifu litakuwa kama _____________.
2. Kusafishwa kwa kanisa kama bibi arusi wa Kristo hakutatimilika mpaka Kristo anapomwakilisha kwake mwenyewe kama kanisa tukufu lisilo na mawaa wala kunyanzi. Hata sasa Kristo anataka kuwasafisha washirika wa kanisa Lake ili

awaandae kwa ajili ya karamu ya arusi ya Mwana Kondoo. Ni mitazamo na utendaji upi upo katika kanisa la leo ambao unaamini Bwana anataka kuundoa wakati anapolisafisna kanisa Lake? ____________________________________.

### V. Sifa za Kanisa kama Mwili

1. Mwili una kichwa ambacho kinauelekeza na kinairatibu mienendo yote ya mwili. Kanisa kama mwili linajinyenyekeza kwa ______________________ ambaye ni Kichwa. Kwa kuwa Kristo ni mkuu na mwenyezi, sisi kama viungo vya mwili Wake tunatakiwa _________________________ kwake Yeye. Uaminifu wetu wa kwanza si kwa viongozi wa kidini bali kwa Kristo. Wakristo wengi wanamchukua Kristo kama Mwokozi wao, lakini kamwe hawajamruhusu Yeye awe Bwana wa maisha yao. Ina maana gani kuwa na Yesu Kristo kama Bwana wa maisha yako? __________________________ ________________________________________________________________.
2. Mwili una viungo vingi, na kila kiungo kinakisaidia kingine. Kila kiungo kinaviitaji viungo vingine vya mwili. Sehemu zote za mwili zinatena kazi, isipokuwa ziwe zinaumwa. Kwa kawaida kiungo cha kanisa kinachoumwa huwa kinatendaje? ______________________________________. Kiungo chenye afya huwa kinatendaje? __________________________________. Kwa kuwa mwili wa Kristo una viungo vingi sana, hauwezi kuwekewa mpaka na kundi moja au dhehebu. Je! tunawezaje kuonyesha kwamba mwili wa Kristo mpaka wake si dhehebu letu? _______________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Sababu ni zipi za kwa nini baadhi ya washirika huwa wanajiondoa kutoka katika mwili?
2. Washirika wengine wanawezaje kufanikiwa katika kuwakaribia hawa?
3. Tunawezaje kuutendea kazi ukuhani wa waamini wote kwa ufanisi zaidi?
4. Tunawezaje sisi kama waamini kuwasaidia wahitaji pasipo kutengeneza utegemezi katika upande wa wale tunaowasaidia kwa vitu? Msaada katika pande zote ni nini?
5. Baadhi ya sifa za Kanisa lililo Mwaminifu kwa Kristo ni zipi? Je! tuko sahihi katika kufikiri kuwa kila lenye kujiita "kanisa" ni lenye uaminifu kwa Kristo? Je! kuna hatari ya kukijumuisha kile ambacho Kristo hakijumuishi? ______________. Je! turuhusu wengine kutokuwa waaminifu kutufanye sisi kuwa tuliopoa na tusioujali uaminifu wetu wenyewe? _____________. Ni nani atakayekuwa mwamuzi wa mwisho? _______________.

## Somo la 13

## Kichwa Cha Mwili

Kanisa ni mwili wa Kristo. Mwili lazima uwe na kichwa ili kuelekeza na kuratibu matendo yake. Katika somo hili tutajifunza jukumu la Kristo kama Kichwa cha Kanisa.

### I. Cheo cha Kristo

1. Kuna rejea mbali mbali katika Biblia ambazo zinamtaja Kristo kama kichwa cha mwili. Soma Waefeso 1:22. Kristo aliyefufuka yu juu ya falme na mamlaka na nguvu na usultani na ameviweka vitu vyote chini ya ____________________ yake. Katika Waefeso 4:15 tunaambiwa kuwa ili tuweze kukua katika mambo yote katika Yeye ambaye ni Kichwa-__________________________, na kulingana na mstari wa 16, mwili wote, ukiwa umeunganishwa na kushikamanishwa na kile ambacho kila kiungo kinaleta, utakuwa umeungana. Kama Kristo anatambuliwa kama Kichwa, basi viungo vya mwili vitafanya kazi pamoja kwa umoja. Tunawezaje kutendea kazi umoja zaidi katika mwili? ___________________________.
2. Katika Wakolosai 1 inatwambia kuwa Kristo ni muumbaji na mtegemezaji wa vitu vyote. Kulingana na mstari wa 18, Yeye ni kichwa cha mwili, __________________, ili kwamba katika mambo yote aweze kuwa _______________________. Kutoka katika nafasi yake ya Ukuu anaweza kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake. Pia Wakolosai 2:10 inasema kuwa sisi ____________________________ katika Yeye, ambaye ni kichwa cha falme na mamlaka yote. Kwa maneno mengine, wakati Kristo ni mkuu katika maisha yetu, ndipo tunakuwa tumetimililka katika Yeye. Kuna wale wenye kufikiri kuwa njia ya kutimilika ni kuwa wa kidini na wa kibinafsi, lakini kulingana na Biblia, twawezaje kuwa tuliotimilika? _______________ _______________________________________________________________.
3. Biblia inafundisha pia kwamba Yesu ni mchungaji mwema na kundi lake ni kanisa. Soma Yohana 10:4. Mchungaji huwatangulia kondoo na kondoo _______________________ yeye maana wanaijua sauti yake. Katika nyakati zingine, Biblia inazungumza juu ya Kristo kama Mwalimu na wafuasi wake kuwa ni wanafunzi. Kwa muhtasari, nafasi ya Kristo ni _____________________ cha mwili, ________________________ wa kundi, na _________________________ wa wanafunzi.

### II. Mfano wa Kristo

1. 1. Kristo aliipata nafasi yake kwa njia ya utii na mateso. Soma Wafilipi 2:5-8. Paulo anatuhimiza tuwe na ________________________ ile ile ndani

mwetu, ambayo ilikuwemo pia ndani ya Krito. Mara nyingi watu wa ulimwenguni huzipata nafasi zao kwa njia ya nguvu na fujo, lakini Yesu hata aliendа msalabani kabla ya kuinuliwa. Kama Yesu alikuwa mwenye kujinyenyekeza sana kwa Baba Yake, isiwe ngumu kwetu kujinyenyekeza Kwake. Kila kiungo/mshirika wa mwili wa Kristo amruhusu Kristo awe mkuu katika maisha yake. Je! Yesu aliipataje nafasi yake ya kuinuliwa?

________________________________________________________________.

2. Katika utii Wake, Kristo alihudumia mahitaji mbali mbali ya binadamu. Soma Luka 4:18-19. Aliwahubiria ____________________ Habari njema, amenitume kuwatangazia wafungwa ______________ ______________, na ______________________ kupata kuona tena, kuwaacha huru ____________________. Inahuzunisha wakati kanisa linajali tu kuhusu wokovu wetu wa baadaye. Yesu aliiwakilisha injili kamili kwa ajili ya mtu mzima. Pamoja na Kristo kama Kichwa cha kanisa, washirika wanafuata mfano wake. Huduma ya kanisa inatakiwa kuhusisha nini?

________________________________________________________________.

3. Katika falsafa ya mtu wa kisasa, mambo ya kiroho yametengwa na mambo ya kimwili. Lakini Yesu hakufanya utengano wa namna hiyo. Soma Mathayo 4:23. Yesu alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, _________________ katika masinagogi yao, na __________________ Habari Njema ya ufalme, na_______________ ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu. Yesu alijulikana kama mtu wa matendo makuu na maneno mbele za Mungu na watu wote. (Luka 24:19)
4. Kwa hiyo tunaona kuwa huduma ya Yesu iljumuisha maneno ya kutamkwa na matendo. Katika ulimwengu wa leo, tunasikia maneno mengi matupu, lakini Yesu alijumuisha kutimilizwa kwa ahadi zake kwa maneno yake. Makubaliano haya kati ya maneno yake na matendo yalileta mamlaka katika huduma yake. Kanisa la leo linakabili jukumu la kuzifuata nyayo za Bwana. Kanisa la leo lilnawezaje kuidhihirisha huduma kama ile ya Yesu?

________________________________________________________________.

## III. Utiii wa Wanafunzi

1. Mwanzoni mwa huduma Yake. Yesu aliwaita wanafunzi Wake. Soma Mathayo 4:19. Yesu aliwaambia, Nifuateni __________________, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa __________________. Kama walikuwa na utayari wa kumfuata Yeye, matokeo ni, watabadilishwa wafanane na Bwana wao. Kuja kwa Yesu ulikuwa ni mwanzo tu wa mchakato wa uanafunzi, ambao ungedumu kwa miaka kadhaa. Wito huu wa uanafunzi una utendaji wa kiinjilisti. Linganisha Mathayo 28:19 na Marko 16:15. Waamini wengi hawaelewi kwamba wanapookolewa na neema ya Mungu, wanaanza katika njia ya uanafunzi. Ni nini mahusiano kati ya uinjilisti na uanafunzi?

________________________________________________________________.

2. Wanafunzi waliiangalia huduma ya Yesu. Waliziona kazi zake na waliyasikia maneno yake. Baadaye walishuhudia kwamba hawakuweza kujizuia kuyanena mambo waliyokuwa wameyaona na kuyasikia (Matendo 4:20). Soma Mathayo 10:25. mwanafunzi anatakiwa awe kama __________________ na mtumishi kama __________________________ wake. Uanafunzi ni mchakato ambapo tabia ya mwanafunzi kwa kuendelea inachukua tabia ya mwalimu wake. Ni wazi kwamba kama mwalimu ni mkuu katika kunena na kutenda, inatakiwa kutarajiwa kuwa mwanafunzi pia atakuwa mkuu katika ____________ na ______________.
3. Ufanyaji wanafunzi wa Yesu haukuwa na mpaka katika nadharia za elimu, lakini ulitekelezwa kwa matendo katika maisha halisi. Soma Mathayo 10:1, 5. Yesu aliwapa mamlaka akawatuma kwenda kufanya kazi. Matokeo yatakuwa ni nini wakati wanafunzi watakapojifunza tu nadharia za huduma darasani? __________________. Tunawezaje kufanikiwa katika kupata mafunzo ya Kikristo ambayo ni mafunzo ya uanafunzi pia? _____________ _______________________________________________________________.

### IV. Muhtasari

1. Nafasi ya Kristo katika ulimwengu ni ile ya Muumbaji, Mtegemezaji na Bwana. Katika kuhusianisha na kanisa, Kristo ni Kichwa cha __________________. Mchungaji wa ________________________ na Mwalimu wa ______________________ Wake.
2. Yesu aliifikia nafasi hii kwa njia ya utii. Aliyahudumia kwa utii mahitaji mbali mbali ya binadamu. Katika tabia yake yalijumuishwa mafundisho yake na kazi zake. Kukubaliana kwa maneno yake na kazi zake kulifanya mamlaka ya huduma yake. Kwa Yesu kulikuwa hakuna utengano kati ya vitu vya kimwili na kiroho.

## Utendaji wa Kikundi

1. Tunawezaje sisi, kama viungo vya mwili, kuwa timilifu katika nafsi zetu na kuwa na umoja katika mwili? Fikiria mtu binafsi na namna za pamoja za hili.

2. Je! mwili wa Kristo wa siku hizi unawezaje kuwa na huduma ambayo ni timilifu na yenye nguvu kama ile iliyoonyeshwa kwa kielelezo na Yesu?

3. Je! mashirika ya elimu ya Kikristo yanawezaje kukutana na changamoto ya uanafunzi wa Kikristo?

4. Kuna mahusiano yapi kati ya uanafunzi na uinjilisti?

# Somo la 14

## Karama za Kiroho

Katika maeneo mengi kuna ubishani kuhusu kamara za kiroho. Ni muhimu kujifunza Biblia ili kujua nafasi na matumizi sahihi ya hizi karama. Karama zatakiwa kuchangia ujenzi wa mwili wa Kristo.

### I. Ya Kuyaangalia Kiujumla

1. Paulo hakutaka washirika wa kanisa Korintho wawe wasiojua kuhusu karama za kiroho. Soma 1 Wakorintho 12:1-2. Walijua vyema jinsi walivyopelekeshwa katika ibada ya sanamu kabla hawajaongoka na kuwa wa Kristo, lakini sasa kama waamini ilikuwa ni muhimu kuwa wanayajua matumizi sahihi ya karama za Roho wa Mungu. Kuna hatua mbili za kuelewa karama: (1) yajue yale ambayo Biblia inayafundisha, na (2) yajue matumizi sahihi ya karama kwa kuzitendea kazi. Kwa namna yako ya kufikiri, je! inawezekana siku hizi waamini hawajui kuhusu karama za kiroho? ________________.
2. Soma mstari wa 3 kwa uangalifu. Inawezekana kuwa katika nyakati zingine waamini Korintho walikuwa wamesikia matamshi yaliyokuwa yamevuviwa kiroho ambayo hayakumtukuza Yesu. Mstari wa 2 unaonyesha kuwa inawezekana kupelekeshwa na roho ambayo si Roho wa Mungu. Kwa sababu hii Paulo anakazia mahusiano ya karibu kati ya kazi ya Roho Mtakatifu na ubwana wa Kristo. Wakati Kristo ni Bwana wa maisha yetu, basi Roho atakuwa na uhuru katika maisha yetu. Pia ni wazi kuwa Roho Mtakatifu anamtukuza ________________________________________.
3. Soma mstari wa 7. Ni mpango na kusudi la Mungu kuwa karama za kiroho ziwe kwa ajili ya washirika wote wa mwili wake na sio tu kundi lililoteuliwa. Hata katika hili, lazima tuwe waangalifu kutokutengeneza kundi maalumu ambalo wanajihesabu wao wenyewe kuwa ni wa "kiroho." Tunajua kuna wale ambao hawajatoa nafasi katika maisha yao katika udhihirisho wa Roho Mtakatifu. Paulo anasema __________________ amepewa udhihirisho/ufunuo wa wa Roho kwa ______________________. Kusudi la udhihirisho ni kuujenga mwili. Ni nini kusudi la karama za kiroho; kuuhudumia mwili wote, au kushawishi watu na kiroho chetu kikubwa? __________________________________________________.
4. Soma mstari 11. Wakati mwingine kuna wale wenye kusema, "Ninazitaka karama, lakini sio hii mahususi." Lakini Roho huzigawa kwa _______________ __________ kama anavyopenda ____________.
   Inawezekana kuwa Roho hazitoi karama zake bure kwa mtu ambaye si mnyenyekevu vya kutosha kupokea karama yeyote anayotaka kuitoa Yeye. Ndipo Roho anadhihirika. Roho ni mwenye-enzi katika hili. Kulingana na

mstari wa 7, tuwe tayari kuzipokea karama zipi? ______________________
_____________________________________________________________.

### II. Yaliyo Maalumu ya Kuyaangalia

1. Mstari wa 8 unataja karama za maneno ya ____________________ na ya ___________________. Lazima tutambue kuwa hizi ni karama za Roho Mtakatifu, na si hasa matokeo ya akili au somo. Zipo nyakati ambapo ndugu au dada mwenye elimu ndogo sana ataeleza neno ambalo linahitajika katika hali fulani. Bila shaka mtu aliye msomi mzuri anaweza kupokea neno kutoka kwa Roho pia. Ili mradi tu kuna mtazamo wa unyenyekevu wa kumtegemea Bwana. Ndugu au dada anapokea habari kimuujiza kwa njia ya maneno ya maarifa, na neno la hekima litatolewa ambalo ndilo hasa linalohitajika katika hali fulani. Je! maneno ya maarifa na hekima ni matokeo ya akili zetu au ni matokeo ya maelekezo ya Roho? ___________ __________________________________________. Andika mfano ambao unaujua wa mtu kutumika katika udhihirisho wa moja ya karama hizi. _____________________________________________________________.
2. Mstari wa 9 unashughulika na karama za ________________________ na _________________. Kila mwamini lazima awe na imani ya kupokea wokovu kwa neema ya Mungu. Lakini karama ya imani inamwezesha mwamini kumtumainia Mungu kwa ajili ya yasiyowezekana. Karama ya imani inaweza kupokewa wakati wa kipindi kigumu cha majaribu, na inamwezesha mwamini kuyavuka majaribu ya moto kwa utulivu na shwari. Yakobo anasema kuwa maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa. (Yakobo 5:15) Karama za uponyaji (ona hili li katika wingi) labda uponyaji wa kimwili, hisia au kiroho. Kwa kuwa Yesu ni Bwana juu ya wote, si ngumu kwa Yeye kuponya katika kila eneo. Wakati ndugu ni mgonjwa, atake shauri kwa nani kwanza; Bwana, au daktari? ________________________.
3. Pia kuna karama ya kutenda miujiza. Muujiza ni tukio ambalo lingekuwa lisilowezekana pasipo Mungu kuingilia kati. Panaweza kuwepo na uponyaji ambayo si hasa miujiza. Mara nyingi miujiza huvunja kile ambacho tunakihesabu kuwa ni sheria za asili. Andika mfano wa muujiza. ________ _____________________________________________________________.
4. Pia kuna karama za __________________________ na ya kupambanua __________________________. Kuna nyakati unabii unachanganywa na kuhubiri. Kiujumla, mahubiri ni ufafanuzi wa Maandiko kutokana na kujisomea, lakini mahubiri yanaweza kujumuisha unabii pia. Unabii ni ujumbe kutoka kwa Mungu unaotolewa katika namna mahususi kuhusu hali fulani wenye matokeo ya mara moja au baadaye. Kanisa linahitaji kuwa na upambanuzi wa roho kwa sababu madhihirisho yote si lazima kuwa yanatoka kwa Mungu. Ndugu wanahitajika ambao wanaweza kupambanua utendaji wa roho mbaya na kuikabili kwa nguvu ya Mungu. Ibilisi

anatamani kuonekana kama malaika wa nuru kwa ajili ya makusudi yake mwenyewe yaliyo maovu. (2 Wakorintho 11:14) Tunawezaje kujua ikiwa unabii au udhihirisho mwingine unatoka kwa Mungu? _________________ ______________________________________________________________.

5. Halafu zimetajwa karama za ________________________________ na ______________________ lugha. Katika sura ya 14, Paulo anaelezea kuwa lugha zinaweza kutumika kwa kujijenga kibinafsi na kwa ajili ya kulijenga kanisa. Mtu mwenye kutumia lugha kuomba au kumsifu Mungu pia anaweza kupokea fasiri. Kama kuna ujumbe wa lugha uliotolewa hadharani, unatakiwa kufasiriwa kwa ajili ya kuujenga mwili. Je! umepata kuyajua matukio ambapo lugha zilitumika pasipo usahihi? _________________. Je! unajua juu ya matukio ambapo lugha na fasiri zililijenga kanisa? _________. Andika maoni yako. __________________________________ ______________________________________________________________.

## III. Muhtasari

Waamini hawatakiwi kuwa wasiojua kuhusu karama. Ubwana wa Kristo na udhihirisho wa Roho vinahusiana kwa ukaribu. Mungu anatamani udhihirisho wa Roho ndani ya kila mshirika wa mwili wa Kristo. Roho Mtakatifu anazigawa karama kama anavyotaka. Ziorodheshe karama tisa za Roho.

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________ .

# Somo la 15

## Kazi ya Kila Kiungo

Katika 1 Wakorintho 12 tunasoma kuhusu udhihirisho wa Roho katika kila kiungo, wakati katika Warumi 12, panazungumza juu ya utendaji wa kila kiungo ndani ya mwili.

### I. Mitazamo ya Lazima

1. Kila kiungo anatakiwa kuwa mwenye kuzielewa sana rehema za Mungu anazozipokea kila siku. Sehemu ya kwanza ya kitabu cha Warumi kinaeleza juu ya rehema za Mungu kama vile: msamaha wa dhambi, njia ya kuufikia uwepo wa Mungu, mwongozo wa Roho Mtakatifu katika maisha yake, na uwezekano wa maisha matakatifu mbele za Mungu. Sasa soma Warumi 12:1. Kwa kuziitikia rehema za Mungu tunatakiwa kuitoa ______________ yetu kuwa dhabihu __________________ takatifu, yenye kukubalika kwa Mungu, ndiyo ibada yetu yenye maana. Ni jambo lenye maana na kueleweka kuwa tuitoe miili yetu kwa Mungu baada ya kupokea mengi sana kutoka Kwake. Tunaweza namna gani kutenda kuitoa miili yetu kwa Mungu? ________________________________________________________.
2. Kuna milinganisho kadhaa katika mstari wa 2. Usifa_________________ na dunia hii, bali ________________________________ kwa kufanywa upya nia zenu. Kwa upande mmoja hatutakiwi kufananishwa na __________________ hii bali tunatakiwa tugeuzwe ili tuweze kuthibitisha mapenzi ya _______________ yaliyo mema na makamilifu. Mageuzi si tu matengenezo ya nje, bali mabadiliko ya msingi ya mitazamo ya ndani ambayo matokeo yake ni namna ya nje ya maisha ambayo itayathibitisha mapenzi ya Mungu. Haiwezekani kutenda kazi vizuri kama kiungo cha mwili wa Kristo pasipo kwanza kulipata hili badiliko la msingi. Ni nini hutokea wakati watu ambao hawajageuzwa wanajaribu kutenda kama viungo vya mwili wa Kristo? ________________________________________.
3. Mstari wa 3 unahusika na tunavyojitathmini. Kulingana na Paulo, hatutakiwi kujifikiria wenyewe ________________ ya vile tunavyotakiwa kufikiri. Kiungo/Mshirika wa mwili anayejifikiria yeye mwenyewe zaidi ya anavyotakiwa ni tatizo. Yeye anajaribu kufanya kila kitu, na anatarajia wengine wajifananishe na njia zake. Lakini mtazamo ulio kinyume pia unaweza kuwepo katika kikundi; nao ni, kuna wale wanajifikira kuwa hawafai. Kwa hiyo mtu wa namna hiyo anapoalikwa ashiriki kwa namna fulani, wakati wote huwa anatafuta udhuru kama vile, “Sina karama kwa hiyo siwezi kulifanya hilo.” Mtazamo huo unazua maendeleo ya kundi pia. Kwa hiyo basi kila mmoja wetu anatakiwa kujifikiria namna gani? Tunatakiwa kujifikiria ______________, kama ambavyo Mungu amempa

kila mmoja wetu kiasi cha ______________. Tunaweza kuisahihisha vipi kila moja ya hii mitazamo? ______________________________________.

4. Tunapochukulia kwa maanani hii halisi kuwa kila kiungo kina kazi katika mwili, tunaweza kuisahihisha hii mitazamo ya kiukuu na kujidharau. Katika mstari wa 9 na 10, tunaona kuwa ufumbuzi ni upendo usio na _________________, upendo wa kindugu. Kuhusu heshima, tunatakiwa ku______________ sisi kwa sisi. Hata kati ya mitume wa Kristo, kulikuwepo na mijadala kuhusu ni nani aliye mkuu kuliko wote. Ni kanuni ya kiroho kuwa yeye ajikwezaye __________, na yeye mwenye kujidhili ______________________.
5. Mstari wa 11-13 unatoa baadhi ya kanuni fupi lakini zilizo muhimu kuhusu utendaji wa viungo vya mwili wa Kristo. Hatutakiwa kuwa ______________ katika shughuli; ________________ katika roho zenu; mkimtumikia___________; kwa tumaini, mkifurahi; katika dhiki, ______________; katika kusali, ______________; kwa mahitaji ya watakatifu, ________________; katika _____________________ mkijitahidi. Je! tunaitendea kazi mitazamo hii? ______________. Ni wapi tunapoweza kupaboresha? ________________________________________.

### II. Kazi ya Viungo/Washiriki Mbali Mbali

1. Ni hakika kuwa kama viungo/washirika wanatendea kazi mitazamo ambayo tumekwisha jifunza, watatenda kazi vizuri katika mwili. Ni nini kitakachotokea katika kusanyiko liliratibiwa vizuri kama viungo/washirika hawana hii mitazamo iliyo ya lazima kuhusiana na utendaji wa mwili? _______________________.
2. Kusanyiko au shirika linaweza kutenda kazi vizuri tu wakati washirika wake wana mitazamo sahihi. Wakati huo huo, ni faida kwa wote wakati washirika wameratibiwa kulingana na kazi ambayo Mungu amempa kila mmoja. Hebu turudi katika mstari 4. Mwili una _________________ vingi lakini si vyote vina ______________________ ile ile. Kulingana na mstari wa 5, Kuna mahusiano mawili: 1) tu mwili mmoja katika _________________________________, na 2) Kila kimoja kiungo kwa ______________________________. Kama tunampenda Kristo, pia tuwapende _________________________, na ili tuwapende ndugu zetu, lazima tumpende ____________________ na kujitiisha Kwake.
3. Soma mstari wa 6. Basi kwa kuwa tuna karama __________________, kwa kadiri ya ___________ mliyopewa; ikiwa ______________, tutoe unabii kwa kadiri ya ___________. Hapa tena tunaona kile ambacho tulikiona katika 1 Wakorintho; kuna karama tofauti na ni zenye mvuto. (Neema linatokana na neno caris) Hapa tena panataja karama ya unabii. Ona kwamba karama zinatakiwa kutumiwa kwa imani. Nini kinatokea kwa karama ambayo haitumiwi? ________________________________________________________.

4. Katika mstari wa 7 kuna zile karama za ________________________ na mafundisho. Huduma, au kuhudumu (diakonia) lina maana pana. Katika 1 Wakorintho huduma mbali mbali za kiroho pia zilikuwa ni diakonia, na katika baadhi ya maeneo, hili linazungumzia kuhudumia meza. Huduma ya Kikristo ni kuhudumia mahitaji yote ya binadamu kwa njia ya neema ya Mungu. Je! unahisi kuwa huduma ya kiroho iwe tofauti na kukutana na hitaji la binadamu? ___________ Je! huduma mbali mbali ziunganishwe kwa jinsi gani? ____________________________________________.
5. Karama ya ualimu inaonekana katika orodha nyingine ya karama pia. (1 Wakorintho 12:28 na Waefeso 4:11) Karama hii ni ya lazima katika maendeleo ya mwili na katika kuwapa mafunzo washirika katika kuzitumia karama zao. Kufundisha ni tofauti sana na kuhubiri. Katika kuhubiri, kweli inatangazwa kwa wasikilizaji, wakati katika kufundisha, kweli inaendelezwa ndani ya wanafunzi. Mafundsho yenye matokeo yanataka ushiriki wa mwanafunzi. Je! kanisa lina mahubiri ya kutosha? __________. Mafundsho ya kutosha? ___________.
6. Mstari wa 8 unataja karama zingine nne: ____________________, ______________________, ___________________ na ____________________. Kuna watu wakarimu ambao wanaweza kuwashirikisha wengine. Mwenye kuongoza anatakiwa kufanya hivyo kwa ______________. Kwa nini? ___________________________________. Kuwa kiongozi (yule mwenye kusimamia) hakutakiwi kuhesabiwe kuwa ni haki bali wasaa. Bidii inaelezewa kama jidihada iliyo makini. Mwenye kurehemu afanye hilo ________________________ na pasipo kuwa na fundo. Karama ya kuonya (kusihi) ni ile ya kufariji na kutia moyo.
7. Ni hakika kuwa mitazamo sahihi ni ya lazima katika mwili kufanya kazi kwa usahihi. Pia ni kweli kuwa wakati kiungo/mshirika wa mwili anapotenda kazi katika karama yake, panatakiwa pawepo na mazingira sahihi ili kuleta mitazamo sahihi. Unaamini lipi ni la muhimu zaidi: kuwa na mitazamo sahihi, au kuwa kila kiungo/mshirika afanye sehemu yake? ____________________________________.

### III. Muhtasari

Ni mitazamo ipi ambayo Biblia inafundisha katika Warumi 12? Fanya orodha ya karama saba zilizoorodheshwa katika sura hii.

## Utendaji wa Kikundi

1. Katika kusanyiko lako, viungo/washirika wanaitendea kazi mitazamo ipi ya Warumi 12? Ni mitazamo ipi inayotakiwa kutendewa kazi zaidi?

2. Tunawezaje kuwasaidia waamini wenye hali ya kujiona wako juu kuliko wengine? Na wale wajionao wako chini kuliko wengine?

3. Jaribu kuzielewa karama zako mwenyewe. Saidia kuzielewa karama za wengine katika kundi.

4. Ni kina nani walio washirika watendaji wa kusanyiko? Ni kina nani wangeweza kushiriki zaidi kama wangekubali kuitoa miili yao kwa Mungu?

# Somo la 16

## Kuwakamilisha Watakatifu

Umejifunza kuwa kila kiungo/mshirika ana kazi yake katika mwili wa Kristo, lakini washirika wanahitaji kuandaliwa kwa ajili ya kazi ya huduma.

### I. Nini maana ya "Kuwakamilisha Watakatifu'

1. Soma Waefeso 4:7-12. Kristo ameweka watu katika kanisa kwa ajili ya kuwaandaa watakatifu. Kauli hii "kuwaandaa watakatifu," ina maana ya ndani sana. Haizungumzii uchoraji wa picha katika kanisa kuu. Haina maana kuwa washirika lazima wawe ni kamili ndipo waweze kumtumikia Mungu. Neno letu "kamili," ambalo linatokana na Kilatini, halikamati maana yote ya neno katartismon, katika Biblia. Neno hili ndilo lililotumika katika Mathayo 4:21 linapozungumza juu ya "kutengeneza nyavu zao." Ina maana kuwa nyavu zilikuwa zikifanywa tayari kwa ajili ya uvuvi. Kwa hiyo tunatakiwa kuwekwa katika utaratibu na kurekebishwa ili tufanye kazi ya Mungu. Kama wanafunzi iliwapasa waziweke nyavu zao katika utaratibu ili wavue, vivyo hivyo maisha yetu yanatakiwa ________________________ ili tuifanye kazi ya Mungu.
2. Lakini huku kuwekwa katika utaratibu hakuzungumzii tu maisha binafsi ya kila mshirika, lakini pia kusahihisha mahusiano katika mwili. Paulo anatumia neno hili hili anapozungumzia umoja wa mwili. Soma 1 Wakorintho 1:10. Amesema, Kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali _____________ katika nia moja na shauri moja. Kwa sababu hii, "kuwakamilisha" au "kuwaandaa" watakatifu maana yake kila mshirika wa mwili yuko katika uhusiano sahihi na ameunganishwa na washirika wengine wa mwili. Mtazamo wa ubinafsi au kuwa huru ni dhambi dhidi ya "ukamilishwaji" au "uandaaji wa watakatifu." Ili kuwa mshirika mzuri wa mwili, lazima tuwe katika maelewano na washirika wengine. Kwa hivyo tunaweza kutenda kazi vyema katika kazi ya Bwana. Tunawezaje kufanya kazi vizuri pamoja? ____________________________.
3. Lakini "kuwakamilisha watakatifu" kunajumuisha zaidi ya kusahihisha maisha yetu binafsi na mahusiano yetu na washirika wengine, lakini pia inahusu Kichwa cha mwili. Soma Luka 6:40. Mwanafunzi hayuko juu ya ____________________ lakini kila mmoja aliye _______________________ atakuwa kama mwalimu wake. Kwa maneno mengine, kuna uhusiano wa karibu kati ya uanafunzi na kuwaandaa watakatifu. Kifungu kile kile katika Waefeso kinataja kuwa kusudi ni kufikia "cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo" (4:13) na kukua katika mambo yote "katika Yeye aliye kichwa –

Kristo" (4:15). Halafu kuwakamilisha au kuwaandaa watakatifu ina maana kwamba tunakua katika kufanana na Kristo zaidi.

## II. Kwa nini "Kuwakamilisha Watakatifu"?

1. Soma Waefeso 4:12 tena kwa uangalifu. Watakatifu wanaandaliwa kwa ajili ya kazi ya ________________ kwa ajili ya ____________________ mwili wa Kristo. Viungo/Washirika wa mwili wanakuwa watumishi katika mwili wa Kristo. Kuna mapokeo katika baadhi ya makanisa ya kumwajiri mchungaji mwenye taaluma hiyo ili aweze kuifanya kazi. Matokeo ya hili ni kwamba tunamlipa yeye ili afanye kazi kwa niaba yetu. Kwa sababu hiyo washirika mmoja mmoja wanaachiliwa huru hata hawafanyi wajibu wao wa kutenda kazi ya huduma. Lakini kulingana na mstari wa 12, watumishi ni kina nani? ____________________________________________.
2. Kazi ya huduma ni yenye upana sana. Hazungumzii kuhubiri kutoka katika madhabahu ndani ya kuta za jengo la kanisa, lakini inajumuisha kazi yote aliyoifanya Kristo na zaidi. Kumbuka huduma kamili ya Kristo katika mahitaji ya binadamu. Yesu alisema hata kazi kubwa zaidi zitafanywa na wafuasi wake (Yohana 14:12). Wewe binafsi unawezaje kufanya "kazi ya huduma"? ____________________________________________.
3. Watati mwingine kuna watu waliowatendaji sana walioridhika na kuwa watendaji tu. Yaweza kuwa kwamba wanajisikia muhimu kuwa na uwezo wa kusema, "Nina shunguli sana." Wakati Biblia inasema kila kiungo/mshirika anatakiwa kuwa na sehemu katika "kazi ya huduma," hili halina maana kuwa kila utendaji ni wenye kufaidisha. Tunahitaji kuelewa utendaji upi ni mapenzi ya Bwana. Uchunguze mstari wa 12. Kazi ya huduma ni kwa ajili ya _______________ ______________________. Kazi ambayo Mungu anaitamani inachangia katika kuujenga mwili. Tunajua kuwa mwli wa Kristo hauna mpaka katika dhehebu fulani, lakini una kipaombele katika mpango wa kimungu. Tunahitaji kuchanganua huduma yetu. Je! utendaji wako unachangia katika kuujenga mwili? _________________. Kwa jinsi gani? Unaweza kwa jinsi gani kukuza ujenzi zaidi wa mwili wa Kristo katika mahali pako? __________________.

## III. Watakatifu wanaweza kuandaliwa na kukamilishwa kwa jinsi gani?

1. Fanya mapitio ya Waefeso 4:7-12. Kristo amelipa kanisa vipawa. Kristo yule yule aliyeshushwa kwa kudharirishwa sasa amepandishwa juu katika Kuinuliwa Kwake. Hili lina maana kuwa Bwana Yesu Kristo ni Bwana wa vyote vilivyoko chini na vyoto vilivyoko juu. Kutoka katika nafasi yake ya kuinuliwa amewapa wanadamu vipawa. Na ametoa wengine wawe _______________, wengine ______________, wengine _____________ na wengine wawe ________________ na waalimu. Kazi ya hawa ni kuwaandaa

watakatifu. Mtume anawasaidia watakatifu kwa kuanzisha makanisa mapya. Nabii anatoa jumbe kutoka kwa Mungu ambazo zafaa katika hali ilipo sasa. Mwinjilisti anaweza kuwapa mafunzo washirika kufanya uinjilisti. Wachungaji na waalimu wanawashauri na kuwafundisha watu wa Mungu. Je! kanisa linatakiwa kuwa na mchungaji? _______________. Aina gani ya mchungaji ni wa kimaandiko zaidi: Yeye mwenye taaluma ambaye anafanya kila kitu, au mtumishi mwenye kuwapa mafunzo washirika wake? __________________.

2. Ni Kristo Mwenyewe aliyetoa wengine wawe mitume, wengine manabii, wengine wainjilisti na wengine wachungaji na waalimu, na anatarajia kuwa watafuata kielelezo chake. Hii ndiyo namna pekee ya wote kuufikia "utimilifu wa Kristo." Kwa hiyo maafisa katika kanisa wapo si kwa bahat mbaya, lakini wapo chini ya mamlaka ya Kichwa cha mwili. Wataweza kuuandaa mwili kwa kufuata kielelezo cha Bwana wao. Yesu amefundisha maneno na matendo. Yesu alikwenda katika uwanda na wanafunzi wake. Leo lazima pia tufundishe halafu tuwaongoze washirika katika kushiriki kutenda katika kazi ya Bwana. Je! unaamini kuwa kufundisha darasani inatosha? Andika maoni yako. ____________________________________
____________________________________________________________.
Itawezekanaje kuandaa washirika wa makusanyiko tofauti? ______________
____________________________________________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Kuwaanda na kuwakamilisha watakatifu kunajumuisha: kuyaweka katika utaratibu maisha yao _________________; kuwa katika makubaliana na ___________________ wengine na kukua katika kufanana na _______________ wetu.

2. Kusudi la kuwaandaa watakatifu ni nini? ____________________. Watumishi ni kina nani? Huduma zao zinaweza kuchangia namna gani katika kuujenga mwili wa Kristo?

3. Kazi ya Mchungaji inatakiwa kuwa ipi? Je! mtu mmoja anaweza kubeba kazi zote za mitume, manabii na wainjilisti? Je! mchungaji anaweza kubeba kazi ya ualimu? Je! kuna watu wengine ambao wanaweza kusaidia katika kufundisha? Washirika wote wanaweza kupokea mafundisho kwa jinsi gani?

## Somo la 17

## Kukihudumia Kichwa

Sehemu ya kazi ya huduma ni kumuhudumia Mungu katika ibada. Ibada ni hatua ya mwanzo ya huduma zingine.

### I. Huduma Tofauti ni Zipi?

1. Soma 1 Wakorintho 12:4-6. Tayari tumeisha ona kuwa kuna karama mbali mbali, lakini mstari wa tano unanena juu ya ________________________ tofauti. Kuna mahusiano kati ya karama na huduma. Karama ni ile inayopokelewa kutoka kwa Mungu ili kuwa na uwezo wa kuhudumia watu wengine. Pia, karama zinamwezesha mtu kuhudumu kwa ufanisi. Huduma inalengwa kwa mtu mwenye karama, kama tu kwa mtu ambaye anahitaji kuipokea faida ya huduma. Lengo la huduma si binafsi, bali faida ambayo wengine wataipokea kutoka katika huduma. Karama inakuja kutoka katika ________________ na huduma ni kwa faida ya ___________________.
2. Katika 1 Wakorintho 12 kuna orodha ya karama mbali mbali, lakini hakuna orodha ya huduma. Hata hivyo, asili ya karama inaonyesha asili ya huduma tofauti. Kwa mfano, katika 1 Wakorintho 14:2, karama ya lugha inaweza kutumika kuzungumza na Mungu, na katika mstari wa 5 panasema kuwa lugha pamoja na fasiri zahudumu kwa kuujenga _______________. Pia, katika mstari wa 22 panasema kuwa karama ya lugha ni kwa ajili ya ishara kwa wasioamini. Kwa hiyo ni wazi kuwa karama inaweza kumhudumia Mungu, kulihudumia kanisa na kuwahudumia wasioamini kulingana na itakavyohusika. Kuna karama zingine ambazo zina matumizi matatu pia. Kwa mfano, karama ya imani inatusaidia kumwabudu Mungu, kulihudumia kanisa na kushuhudia ulimwengu. Kwa hiyo huduma tofauti zaweza kuhudumia ______________________, kuhudumia _________________ na kuwahudumia _______________________. Somo hili linahusu zaidi kumhudumia Bwana wakati somo lililopita linahusika na huduma kwa kanisa na ulimwengu.

### II. Inawezekanaje Kumhudumia Mungu?

1. Kwa namna moja, hatuna chochote cha kumpa Mungu. Yeye ni mwenye kujitosheleza katika nafsi yake mwenyewe. Lakini wakati huo huo, Biblia inasema kuwa washirika wa kanisa la Antiokia walimhudumia Bwana. Soma Matendo 13:2-3. Kati yao walikuwepo manabii na waalimu waliokuwa wakishiriki katika kufunga na maombi. Kumbuka kulingana na Waefeso 4, manabii na waalimu ni zawadi kwa kanisa kutoka kwa Mungu Kwa hiyo waliweza kumhudumia Bwana kwa sababu walikuwa wamepokea

kutoka ________________. Ukweli ni kuwa kila karama njema na kamili hushuka kutoka juu. (Yakobo 1:17) Basi kitu pekee chema ambacho tunaweza kumpa Bwana ni kile ambacho tumepokea kutoka Kwake. Baadhi ya karama njema ulizozipokea kutoka kwa Bwana ni zipi? _______
___________________________________________________________.

2. Ni kimantiki kuwa sehemu ya huduma yetu kwa Bwana ni kumpa Yeye shukrani kwa ajili ya karama njema alizotupa. Karama za Mungu ni madhihirisho ya neema ya Mungu, na katika kuipokea neema ya Mungu tunampa Mungu shukrani. Wakati mwingine hatuna shukrani sana, hatutoi shukrani kwa ajili ya mambo mazuri na hata kufikiri kuwa kile ambacho tunakipokea si kizuri. Soma Waefeso 5:20. Inasema __________ Mungu Baba sikuzote kwa _________, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo. Kulingana na Biblia, tunatakiwa kutoa shukrani hata kwa kile ambacho hakionekani kuwa ni chema. Je! unaamini kuwa tunatakiwa kushukuru kwa ajili ya mambo yote? _________________.
3. Huduma yetu kwa Mungu ina sehemu ya kiroho. Soma Yohana 4:24. Wale wenye kumwabudu Mungu yawapasa kumwabudu Yeye katika ____________ na katika ________________. Paulo anaandika katika 1 Wakorintho 14:15 kuwa aliomba na aliimba katika Roho na kwa ufahamu. Katika Warumi 8:26, panasema kuwa Roho anatuombea kwa ___________________ kusikoweza kutamkwa. Ili kuwa na ushirika na Roho wa Mungu, roho zetu lazima ziwasiliane na Mungu. Mzizi wa tatizo letu ni nini wakati hatutaki kumsifu Bwana? _______________________.
4. Lakini ibada haina mpaka katika uwanda wa kiroho. Kumbuka kuwa tunatakiwa kuabudu katika roho na katika kweli. Kuimba kwetu na kuomba kunatakiwa kuwa katika roho, lakini katika kweli pia; na kuimba kwetu na kuomba kunatakiwa kuwa kwa Roho na pia kwa ufahamu. Kile ambacho kinafanyika katika roho kinatafsiriwa katika utendaji. Tunapomwabudu Mungu katika roho, inatakiwa kutarajiwa kuwa tunautendea kazi uwepo wa Mungu katika maisha yetu ya kila siku. Paulo anaandika juu ya ibada yenye maana katika Warumi 12:1. Tumepokea rehema nyingi sana kutoka kwa Bwana hata ni juu yetu sisi kuitoa _______________ iwe dhabihu iliyo hai. Dhabihu hii haifanyiki tu katika majengo ya kanisa lakini katika kila mahali tunapokwenda. Tunawezaje kuitoa miili yetu kwa Bwana kila siku? ____________________________
___________________________________________________________.

### III. Ni nini Matokeo ya Huduma Yetu kwa Mungu?

1. Katika Matendo 13 tunaambiwa jinsi ambavyo walimhudumia Bwana, na matokeo yake Roho Mtakatifu akawaambia Barnaba na Sauli wanatakiwa kufanya nini. Matokeo yake wakatumwa waipanue kazi ya Bwana katika maeneo mengi. Baada ya kumsifu na kumwabudu Bwana, inawezana kuwa

Bwana atatutumia kwa ufanisi zaidi. Katika safari zake za umishenari, Paulo alitumika kwa nguvu kufanya miujiza na kuhubiri Neno. Tunapomhudumia Mungu kwa kuabudu, Mungu anawahudumia watu Wake kwa nguvu. Kipi kitangulie – utumishi au ibada? __________________________.

2. Katika 2 Wakorintho 3, Paulo anaielezea huduma ya agano jipya. Chini ya agano jipya, palikuwepo na utaji uliofunika uso wa Musa, lakini katika agano jipya, kwa nyuso zisizofunikwa tunautazama utukufu wa Bwana. Soma mistari wa 16-18. Ili kumwabu Mungu tunahitaji kuuona utukufu wa Bwana. Kwa njia hii Roho anatuweka huru kutoka katika vizuizi vyenye kuzuia sifa zetu. Kulingana na mstari wa 18, ni nini matokeo ya kuutazama utukufu wa Bwana? Tuna_____________ toka utukufu _______________ kuwa katika mfano ule ule. Hili linatwambia sisi kuwa ibada ya kiroho matokeo yake yatakuwa mabadiliko endelevu yenye kutuleta sisi kuwa katika mfano wa Kristo. Hata saikolojia inatufundisha kuwa tunaanza kufanana na kile tunachokitazama. Kama tukiendelea kutazama mambo maovu, tunaweza kufanana nayo. Lakini kama tukikaza macho yetu katika kuutazama utukufu wa Mungu, tutafanana zaidi na __________________.
3. Hili linakubaliana na yale anayoyafundisha Paulo katika Waefeso 4. Kazi ya huduma ni ili kwamba mwili ujengwe hadi kufikia mahali ambapo wote watakua na kufikia ___________________________ cha utimilifu wa __________________________. Kama ibada ya kweli inatendewa kazi, basi tutasonga mbele katika kufanywa kuwa katika mfano wa Kristo. Je! kanisa linatenda aina hii ya kuabudu siku hizi? _________________. Tunawezaje kuitenda kwa ubora zaidi ibada ya kweli? __________________________.

.

## Utendaji wa Kikundi

1. Kuna mahusiano gani kati ya karama na huduma?

2. Matokeo yatakuwa ni nini kama tukianza kutoa shukrani kwa ajili ya mambo yote?

3. Unamshukuru Mungu kwa ajili ya mema yapi?

4. Unamshukuru Mungu kwa ajili ya mambo gani yasiyokuwa na makubaliano?

5. Ina maana gani kuomba na kuimba katika Roho?

6. Shirikishaneni kuhusu kuitoa miili yetu kwa Bwana kila siku.

7. Ni mada zipi ambazo huwa tunazungumza na marafiki zetu zaidi? Nini kitatokea kama tunazungumza zaidi kuhusu mambo ya Mungu?

# Somo la 18

## Huduma kwa Mwili

Kukihudumia Kichwa, au kuabudu, ni maandalizi ya huduma kwa mwili. Huduma kwa mwili inajumuisha karama ambazo Mungu ameziweka katika mwili, na karama hizi kutumiwa na viungo vya mwili katika kuhudumiana.

### I. Tunawezaje Kuuhudumia Mwili?

1. Viungo/washirika wote wa mwili wana mahitaji binafsi. Kama wote tunasubiri kupata faida kutoka katika huduma za wengine, basi hapatakuwepo na yeyote wa kuwahudumia wengine. Kuna tofauti kubwa kati ya kuwa "kimelea" na mtumishi. Kimelea anatarajia kupokea tu, wakati mtumishi anataka kushirikisha. Ni nini tofauti kati ya mshirika kimelea na mshirika mwenye kuhudumia? ____________________________________.
2. Ili kuwa na uwezo wa kuhudumu, lazima kwanza tupokee. Neema ya Mungu ni chanzo cha huduma zetu. Kiungo/Mshirika anayejaribu kuhudumu pasipo neema ya Mungu hakika atafeli. Katika 1 Wakorintho 12, karama zimetajwa kwanza, ndipo huduma, halafu, utendaji. Mtu lazima apokee kutoka kwa Mungu ili aweze kuwashirikisha wengine. Ni nini kitatokea kama tunajaribu kuhudumu pasipo msaada wa Mungu? ________ ____________________________________. Basi tunawezaje kuhudumu? ____________________________________________________________.
3. Ni kwa ajili ya faida yetu kuutazama mfano wa kanisa la mwanzo. Katika siku ya Pentekosti, wanafunzi walishuhudia juu ya nguvu ya Mungu kwa njia ya uwezesho wa Roho Mtakatifu. Walinena juu ya kazi za ajabu za Mungu (Matendo 2:11). Na watu wengi waliongezwa katika kanisa (mstari wa 41). Soma mstari wa 42. Wakawa wakidumu katika_____________ la mitume, na katika _______________, na katika kuumega mkate, na katika _________________. Baada ya kumhudumia Mungu kwa maombi na sifa, Mungu aliwafanya kuwa na uwezo wa kuwahudumia wengine kwa njia ya vitu na pia kiroho. Ni nini kitakachotokea kama mtu anajihesabu ametingwa sana katika kuhudumu hata anasema hana muda wa kumsifu Mungu? ____________________________________________________.

### II. Tunawezaje kuyahudumia mahitaji ya binadamu?

1. Mfano wa kanisa la mwanzo utatusaidia sisi kupata njia yetu katika hili. Soma Matendo 2:43-47. Siku hizi kuna makundi yenye kusisitiza huduma ya kiroho peke yake, wakati kuna makundi mengine ambayo yanasisitiza upande wa vitu vya kimwili na kijamii. Lakini bidii ya kanisa la kwanza

liliziunganisha hali zote hizi mbili katika huduma moja. Katika mstari wa 43 tunasoma kwamba mitume walifanya ________________________ na ishara, wakiidhihirisha nguvu yao ya kiroho. Halafu katika mstari wa 45 unatwambia sisi kuwa wote walioamini waliuza _____________________ na vitu wakavigawa kati ya wote, kadri ya mtu yeyote alivyokuwa na _________________. Kulingana na mstari wa 46 walikuwa _________________ kila siku, wakimega mkate kutoka ________________.

2. Soma mstari wa 47. Unasema walikuwa ___________________ Mungu, na ______________________ watu wote. Sifa yao ilikuwa na sifa ya nguvu ya kiroho iliyowafikia watu, hilo ni, lilikuwa na hali ya kijamii. Haishangazi kuwa Bwana _______________________ kanisa kila siku. Kanisa linaweza kukua linapopalilia maisha katika Mungu hadi kufikia mahali watu waliolizunguka wanakuwa wenye kupata kufaidika kutoka katika upendo wao wa Kikristo. Je! inawezekana kumsifu Mungu na tusiwasaidie watu waliotuzunguka? __________________. Je! inawezekana kwa mtumishi wa Bwana kuwasaidia watu pasipo kushuhudia kuhusu Mungu? ____________________. Fikiria kuhusu majibu yako. Tunawezaje kutenda huduma yenye kuunganisha yote hali ya kiroho na ya vitu vya kimwili? _____________________________________________________________.

3. Katika sura ya 3 kuna mfano mwingine wa huduma kwa mahitaji ya binadamu. Palikuwepo na mtu kiwete aliyekuwa akiomba katika lango la hekalu. Inaonekana kwamba watu wengi walifikiri kuwa kiwete alihitaji sadaka tu. Lakini Petro alipofika, alimpa mtu huyu kitu fulani chenye thamani zaidi. Soma Matendo 3:6-7. Petro hakumpa fedha; alimpa uponyaji kwa njia ya nguvu ya Mungu. Hitaji dhahiri ni hitaji la hela, lakini hitaji la ndani sana la mtu huyu lilikuwa ni uponyaji. Ni rahisi kutosheka tu kuhudumia mahitaji dhahiri na kuyaacha mahitaji ya ndani sana hayajaguswa. Ni mahitaji baadhi yapi yaliyo dhahiri waliyonayo watu? ________________. Baadhi ya mahitaji yao ya ndani sana ni yapi? _____________________________________________________________.

4. Wakati mtu aliyepooza alipoponywa, alianza kumsifu Mungu. Soma Matendo 3:8-9. Aliingia hekaluni akitembea, akiruka, na kumsifu _________________ na _________________ walimwona. Hapa tunaona mzunguko wa sifa. Kwanza, kanisa lilimsifu Mungu; halafu nguvu ya Mungu ilidhihirishwa; halafu wapokeaji wa huduma iliyojaa nguvu walimsifu Bwana. Kama tukihudumu kwa nguvu zetu wenyewe, tunapokea sifa, lakini kama tunahudumu kwa nguvu ya Mungu, anapokea Yeye utukufu. Ni maoni gani ambayo watu huwa wanatoa kuhusu kanisa letu? _____________________________________________________________.

**III. Matakwa ni yapi ili kuwa na uwezo wa Kuhudumu?**

1. Kanisa lilikabili tatizo kuhusu wajane wa Kiyunani. Ni dhahiri palikuwepo na ugawaji wa kila siku wa mahitaji. Palikuwepo na matakwa yaliyoelezewa vyema kwa wale waliokuwa wameteuliwa kugawa haya mahitaji. Soma Matendo 6:3. Walitakiwa kuchagua watu saba wa kundi lenye kushuhudiwa ________________________, waliojaa ________________________ na ____________________. Je! unafikiri kanisa la leo linatakiwa kuwa na matakwa yale yale? _____________.

2. Katika 1 Wakorintho 12-14 kuna baadhi ya maelekezo. Katika 12:7 tunaambiwa kuwa udhihirisho/ufunuo wa Roho unapewa kwa ___________________________ wote. Katika 12:22, tunaambiwa kuwa viungo/washirika wa mwili ambao wanaonekana kuwa ________________________ ni wa muhimu. Katika sura ya 13, imeeleweshwa kuwa matumizi ya karama za Roho yanaweza kuwa tupu na yasiyo na maana pasipo ___________________. Katika 14:12 Paulo anasema tunatakiwa kutamani sana karama za ______________, na kwa ajili ya _______________ kanisa. Pia, anahimiza kuwa washirika wote wanatakiwa kushiriki (14:26-27). Mwisho, Paulo analielekeza kanisa kuwa wanatakiwa kutamani sana kutoa unabii, na wasikataze kunena kwa lugha; bali wafanye mambo yote kwa __________________ na ___________________. Jibu swali hili kwa maneno yako mwenyewe: Ni mtazamo upi ulio sahihi wa kuzitenda karama na huduma? ____________________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Washirika walio vimelea wanawezaje kubadilika na kuwa washirika wenye kuhudumia wengine?

2. Toa baadhi ya mifano ambapo washirika wa kanisa wamejumuisha kwa mafanikio huduma ya kiroho pamoja na kukutana na mahitaji ya kimwili?

3. Je! tunahudumia mahitaji yaliyo dhahiri au mahitaji ya ndani sana ya watu? Tunawezaje kuhudumia kwa ubora mahitaji yao ya ndani sana?

4. Pamoja na kundi mchanganue maoni ya jumla ambayo watu huyatoa kuhusu kusanyiko lenu la mahali. Ni nani anayepokea kutambuliwa?

5. Ni matakwa yapi ndiyo ya muhimu zaidi kwa wale ambao watahudumu kwa njia za kiroho na kimwili?

# Somo la 19

## Huduma Yetu kwa Ulimwengu

Katika masomo yaliyopita umejifunza kuhusu huduma ya mwili kwa kichwa na kwa viungo/washirika wengine wa mwili. Katika somo hili, jifunze kuhusu huduma ya mwili wa Kristo kwa ulimwengu.

### I. Mfano wa Kristo kwa Ulimwengu

1. Yesu aliiacha nafasi yake iliyoinuliwa katika utukufu ili awatumikie binadamu katika ulimwengu huu. Soma Wafilipi 2:5-8. Alikubali kijidhili na hata kuteseka ili atumikie. Mara nyingi watu wanafikiri kuwa lazima tupande hadi kufikia nafasi ya juu ili kuweza kutumikia wengine. Je! ni lazima kuwa na nafasi iliyoinuliwa ili kutumikia? ____________________.
2. Hata ingawa Yesu alijidhili Mwenyewe, wakati huo huo alikuwa ni nuru ya ulimwengu (Yohana 8:12). Linganisha Mathayo 5:14. Kwa hiyo wale wenye kumfuata Kristo pia wanaweza kuwa ____________________ ya ____________________. Tazama Mathayo 5:16. Nuru yetu inatakiwa kuangaza sana mbele za watu ili wayaone ___________ ___________ yetu na kumtukuza Baba yetu aliye mbinguni.
3. Yesu alikuwa mkuu wa matendo na maneno. Aliwafundisha, alihubiri na kuponya watu. Mathayo 4:23. Alisema injili hii itahubiriwa katika ulimwengu wote. Mathayo 24:14. Alimshukuru Baba kwa ajili ya watu aliompa Yeye kutoka ulimwenguni (Yohana 17:6). Wakati wanaume na wanawake wanatoka ulimwenguni na kuja kwa Kristo, mwili wa Kristo unakua. Kulingana na mistari hii, tunatakiwa kuhubiri injili wapi? ______________________. Matokeo ya kuhubiri kwetu yanatakiwa kuwa nini kwa watu wa ullimwengu huu? ______________________.
4. Mafundisho ya Yesu yalikuwa kwa neno na mfano. Yesu aliwaita wanafunzi wamfuate Yeye ili waweze kuona na kusikia yale aliyoyafanya na kusema. Mafundisho yake yaliwaonyesha njia ya kutenda haki na upendo katika mahusiano yote ya kibinadamu. Wanafunzi waliona jinsi ambavyo Yesu alitatua matatizo waliyoyaleta kwake. Halafu Yesu aliwatuma wafanye kama ambavyo Yeye alikuwa anafanya. Mwanafunzi wa Yesu anafanya nini? ____________________________________.
5. Mbali na kufundisha na kuhubiri, Yesu aliponya watu wengi. Alitoa mapepo, aliwapa kuona vipofu na alifufua wafu. Uponyaji ulikuwa ni wa kiroho kama tu ulivyokuwa ni wa kimwili. Miujiza ya uponyaji ililithibitisha neno lililotangazwa. Yesu aliponya watu ________________________ na pia kimwili.
6. Mungu ana njia nyingi ya sisi kuhudumia kwa ufanisi mahitaji ya binadamu. Mungu anabariki kazi ya madaktari na manesi. Lazima

washirikiane na sheria za afya ambazo Mungu ameziweka ili uponyaji uje katika miili yenye magonjwa. Lakini si magonjwa yote huitikia matibabu ya kidaktari. Kuna magonjwa ambayo hayawezi kuponywa kwa njia za asili. Mungu anaweza kuponya magonjwa yote na maradhi, yawe yana chanzo cha asili au cha kiroho. Kiungo/Mshirika wa mwili wa Kristo anawezaje kuhudumia wagonjwa siku hizi? ____________________________________
________________________________________________________________.

## II. Agizo la Kristo kwa Ulimwengu

1. Maneno ya mwisho ya Kristo kabla hajaondoka katika huu ulimwengu yanaonyesha agizo ambalo tunalitumikia katika huu ulimwengu. Mathayo 28:19 inasema, mkawafanye ____________________ yote kuwa wanafunzi. Marko 16:16 - Mhubiri Injili kwa ____________ kiumbe. Yesu hataki sisi tujali tu mambo ya ndani ya kanisa, bali tutoke tufanye kazi katika ulimwengu huu. Ni nini kitakachotokea kama kanisa linajijali tu lenyewe? ________________________________________________________________.
2. Yesu pia aliwaamuru wanafunzi wangojee Yerusalemu mpaka wapokee nguvu ya Roho Mtakatifu. Luka 24:49. Baada ya kujazwa na Roho, walishuhudia juu ya Kristo Yerusalemu na katika miisho ya nchi. Matendo 1:8. Waliweza kuifanya kazi ya Mungu kwa sababu walikuwa na nguvu ya Mungu katika maisha yao. Hata leo ni nguvu ya kiungu ya Mungu ndiyo yenye kuifikisha kazi ya Mungu. Tunapokea wapi nguvu ya kuwa mashahidi katika huu ulimwengu? ______________________________.
3. Mfano wa Yesu unathibitisha agizo Lake. Yesu amesema katika Yohana 17:18 kwamba Baba amemtuma, na akawa anawatuma wanafunzi ulimwenguni. (Pia Yohana 20:21.) Mungu aliupenda sana ___________________________ hata akamtoa Mwanawe wa pekee. Baba alimtoa Mwanawe wa pekee, na Mwana akautoa uhai wake kwa ajili ya ulimwengu uliopotea. Je! tunatenda aina hii ya upendo? ________________. Je! tunawezaje kufanya hilo bora zaidi? ________________________________________________________________.
4. Sasa tunajua kile ambacho Yesu ametutuma kufanya. Kama tunampenda Yeye tutafanya kile ambacho ametuamuru kufanya. Amesema kuwa tufanye wanafunzi, tuhubiri injili, na tutatumwa jinsi ile ile ambayo alitumwa Yeye. Yote haya yanaonyesha kuwa ni juu yetu kuishi kama alivyoishi Yeye na kwa namna hiyo kuiendeleza kazi Yake. Siku hizi kuna wengi wenye wasiwasi kuhusu hali zilizomo duniani, lakini wanajaribu kuyatatua matatizo ya ulimwenguni pasipo kufanya kama alivyofanya Kristo. Matokeo yatakuwa ni nini kama tunafikiri tunaweza kutatua matatizo kwa kutumia tu njia za kibinadamu? ____________________________________________.

   Nini kingetokea ulimwenguni kama Wakristo wote wangeendeleza kazi ya

Kristo kwa nguvu ya Roho Mtakatifu? ______________________________
_______________________________________________________________.

**III. Muhtasari**

1. Yesu aliweka mfano kabla yajatoa agizo. Alipaacha mahali pake katika utukufu ili ateseke na kuuhudumia ulimwengu huu wenye mahitaji. Kwa njia ya mafundisho, mahubiri na uponyaji akawahudumia binadamu. Baadhi ya watu wametoka ulimwenguni ili wawe viungo/washirika wa mwili wa Kristo unaokua. Ni juu ya wafuasi wa Kristo kuiendeleza kazi aliyoianza. Ni nini mahusiano kati ya yale tunayoyahubiri na yale tunayotenda? ________________________________________________.
2. Baada ya kuweka kielelezo, Yesu alitoa agizo Lake. Maneno yake ya mwisho katika dunia hii yanaonyesha shauku yake ya kuukomboa huu ulimwengu. Amewaagiza wafuasi wake wafanye wanafunzi zaidi, wahubiri injili na washuhudie kwa nguvu ya Roho. Amelijumuisha hili kwa kusema, “Kama Baba alivyonituma mimi, vivyo hivyo ninawatuma ninyi.” Kama Wakristo, je! tusubiri tutumwe, au tumeisha tumwa? ___________________________
_______________________________________________________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Yesu amefundisha, kuhubiri na kuponya. Yapi kati ya haya matatu ndiyo tunayoyafanya zaidi? ______________________. Yapi ndiyo tunayoyafanya kidogo? ______________________________.

2. Matendo yapi mema yangeweza kuwa nuru ulimwenguni na kumtukuza Mungu? ______________________________________________.

3. Tutake shauri kwa nani kwanza tunapokuwa tu wagonjwa? ____________________________.

4. Maagizo ya mwisho ya Yesu yalikuwa ni yapi? Mfanye ____________________________, mhubiri ____________________, mvikwe na ________________________________.

5. Je! tunayatii haya maagizo, au tuko tunashughulika kufanya mambo mengine? ____________________________.

# Somo la 20

## Ukomavu Katika Kristo

Baada ya kuandika kuhusu huduma, Paulo aliwaandikia Waefeso kuhusu ukomavu katika Kristo.

### I. Hitaji la Ukomavu

1. Baada ya mtu kuja kwa Kristo, anahitaji kulishwa kiroho. Soma 1 Petro 2:2. Kama watoto wachanga tunatakiwa kutamani __________________ ya kiroho ili tuweze kukua. Mtoto anatunzwa na mtu aliyemzaa. Kwa hiyo viungo/washirika wa mwili wa Kristo wana wajibu kuwalisha na kuwatunza viungo/washirika wapya. Ni ajabu wakati kila mshirika aliyekuwa mtu mzima anamtunza mshirika mchanga. Je! umewahi kupata uzoefu wa kutunza mshirika mchanga? _______________.
2. Mtoto mwenye kukua anajifunza kujilisha mwenyewe. Soma Matendo 17:11. Watu wa mji wa beroya walilisikia Neno la Paulo likihubiriwa wakaenda katika nyumba zao wakayachunguza ____________________. Mtoto ambaye hajifunzi kamwe kujilisha mwenyewe atakua pole pole sana. Kama wao, kuna Wakristo ambao hawaendelei kamwe kwa sababu wakati wote wanasubiri mtu mwingine awape chakula cha kiroho. Je! unaamini waberoya walikuwa kiroho? ___________________ Kwa nini? _________ ____________________________________________________________.
3. Mwamini mpya anatakiwa kukua katika neema ya Mungu. (2 Petro 3:18) Wakristo hawatakiwi kuendelea tu kunywa maziwa. Soma Waebrania 5:12-14. Kulingana na ujumbe huu, wale ambao wamefundishwa wanatakiwa waanze kuwafundisha wengine. Wale walioshiriki maziwa peke yake wanatakiwa kukua ili waweze kumeng'enya chakula _________________________. Katika sura inayofuata katika Waebrania, panaeleza jinsi ya kuendelea hadi ukamilifu, au ukomavu.
4. Tunaweza kutolea mfano ukomavu kwa kutumia mlinganisho kati ya mkokoteni na gari. Mkokoteni unaweza kwenda tu wakati mtu fulani anausukuma. Wakati hakuna mtu anayeusukuma, unakua umesimama pale pale. Lakini gari linabeba mzigo, na hata linambeba dreva. Mkristo ambaye hajakomaa mara nyingi huwa anasubiri mpaka mtu fulani ampe hamasa, wakati mshirika aliyekomaa ana uwezo wa kujipa hamasa mwenyewe na pia anatia moyo wengine. Mkristo aliyekomaa hasubiri tu msaada kutoka kwa wengine, lakini anajitoa kuwasaidia wengine. Washirika wengi wa kanisa lako la mahali wamefikia hatua gani ya ukomavu? ___________________ ____________________________________________________________.

## II. Hatua za Ukomavu

1. Sasa tunarudi katika Waefeso 4. Kumbuka kuwa tumejifunza kwamba viongozi wa kanisa wanatakiwa kuwapa mafunzo washirika kwa ajili ya kazi ya huduma. Wanakua kwa sababu wanafanya kazi kwa ajili ya Bwana. Mwili wetu wa kibinadamu unakua wenye nguvu kwa njia ya mazoezi. Soma Waefeso 4:13. Tunahitaji kufikia ___________________ wa imani na ____________________________ Mwana wa Mungu. Hisia ya umoja kati ya ndugu ni namna moja ya kumjua Kristo bora zaidi. Nini kitatokea katika kanisa pale ambapo hakuna umoja? _________________________ ________________________________________. Je! litakua? _________.
2. Pia wanatakiwa kukua katika kumjua Bwana Yesu Kristo. Hili halizungumzii uwezo wa kiakili, bali uhusiano binafsi na Kristo. Kulingana na mstari wa 13, tunatakiwa kukua hata kufika kwenye cheo cha kimo cha __________________ wa Kristo. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wajifunze kwake maana alikuwa mpole na mnyenyekevu wa moyo. Mkristo mwenye kukua anatamani utu wake uwe kama Yesu kila siku. Je! unamjua yeyote ambaye yuko kama Kristo hasa? _______________. Wote lazima tuendelee kusonga katika hili. Je! unataka kufanana na Kristo zaidi. Omba na kutaka msaada wa Mungu. Ili kukua na kuwa kama Yeye, lazima tuendelee kumtazama Yeye. Kulingana na Waebrania 12:2, tunatakiwa kumtazama ______________________. 2 Wakorintho 3:18 inatwambia tunapoutazama utukufu wa Mungu, tunabadilishwa toka utukufu hadi utukufu.
3. Wakati viungo/washirika wote wanakuwa kama Kristo zaidi, hawaangukii katika mafundisho ya uongo na upotovu. Soma mstari wa 14. Kristo hataki sisi tuwe kama watoto, tukiyumbishwa huku na kule na kila ______________ wa mafundisho. Mara nyingi inatokea kwamba washirika wasio komaa ndio wanaoweza zaidi kuangukia katika upotovu. Wale wanaomtumikia Bwana kwa uaminifu wana nguvu zaidi na msimamo zaidi. Mara nyingi kuna washirika ambao ni dhaifu kwa sababu hawatumii karama ambazo Mungu amewapa. Je! kuna washirika walio dhaifu katika kanisa? _______________. Wanaweza kutiwa nguvu kwa jinsi gani? _____ ____________________________________________________________.
4. Hatua nyingine kuelekea katika ukomavu ni kuitangaza kweli. Upotovu unashindwa kwa njia ya kweli. Soma mstari wa 15. Wakristo waliokomaa wananena kweli kwa upendo. Mtu asiyekomaa ananena kweli kwa namna yenye kukwaza. Halafu kuna wale wanajisikia kutokunena kweli kwa upendo, kwa sababu wanaogopa. Lakini Paulo anasema mwili uta____________________ wenyewe kwa ____________________ (mstari wa 16).

5. Soma mstari wa 15 na 16. Wakati viungo/washirika wa mwili wameunganishwa na kichwa, ambacho ni Kristo, viungo/washirika wa mwili wataunganishwa pia. Viungo vitafungamanishwa na kuunganishwa. Wakati mwingine kuna watu wanaokiri kuwa wameunganishwa na Kristo, lakini hawataki kujiunga na mwili wa Kristo. Katika moja ya nyaraka zake, Yohana anasema kuwa kama tunampenda Mungu tutawapenda ndugu zetu pia. Ndugu wanawezaje kufanya kazi pamoja? ______________________
______________________________________________________________.
6. Utendaji wa kila mtu mmoja mmoja inachangia ukuaji wake. Wakati kila kiungo/mshirika anapofanya sehemu yake, kanisa linakua. Kuna wale wenye kulishutumu kanisa, lakini wao wenyewe ndiyo wanaoweza kukwamisha au kusaidia ukuaji wa kanisa lao. Kulingana na mstari wa 16, lengo letu si kujitosheleza binafsi, wala si kwa kanisa kuwa vyema peke yake, bali ukuaji ambao utaleta watu wapya kwa Kristo. Unawezaje wewe kulisaidia kusanyiko lako mwenyewe kukua? ______________________
______________________________________________________________.

### III. Muhtasari

1. Viungo/Washirika wapya wa mwili wanahitaji chakula ili wakue. Watu wa beroya walijifunza Maandiko wao wenyewe. Baada ya kufundishwa, tunatakiwa tuwafundishe wengine. Baada ya kunywa maziwa kwanza, tunakuwa na uwezo wa kula chakula kigumu. Je! unaamini washirika wa kusanyiko lako wanakua? ____________.
2. Waefeso 4 inawakilisha hatua za kukomaa: 1)Washirika wote wa kanisa lazima wapewe mafunzo ya kutumikia. 2) Kila Mkristo anatakiwa kufanana na Kristo zaidi. 3) Wakristo walikomaa wanatakiwa kuyakabili mafundisho ya uongo. 4) Viungo/Washirika wa mwili wananena kweli kwa upendo ili kuujenga mwili. 5) Kanisa litaendelea kukua wakati kila kiungo/mshirika anafanye sehemu yake. Je! kusanyiko lako linakua? Je! linakua kwa kasi au pole pole? __________________.

## Utendaji wa Kikundi

1. Je! tunawezaje kusaidia mtu binafsi kujifunza Biblia?

2. Tatizo letu la msingi ni nini; ukosefu wetu wa nguvu, au kufeli kutendea kazi umoja?

3. Tunawezaje kufanikisha ukuaji na maendeleo katika washirika wote?

4. Ni mambo gani yenye kuchangia ukuaji katika kusanyiko?

Imetafsiriwa na Nkongi Emmanuel Kamwela
Imehaririwa na Stacy Collins
Imechapishwa na Mizizi Mobile Missions Press © 2020

Foursquare Missions Press

The Way of Discipleship — Swahili
Foursquare Missions Press @2005